JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

## HOTUBA YA MHESHIMIWA JUDITH SALVIO KAPINGA (MB.), WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/2027




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, (wa pili kutoka kushoto); Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe Judith Salvio Kapinga (wa kwanza kulia), na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, Mheshimiwa Prof. Riziki Silas Shemdoe, (wa kwanza kushoto) katika hafla ya uzinduzi wa soko jipya la Kariakoo Dar es Salaam uliofanyika tarehe 9 Februari, 2026 Jijini Dar es Salaam.*

**DODOMA** **MEI, 2026.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA JUDITH SALVIO KAPINGA (MB.), WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/2027




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, (wa pili kutoka kushoto); Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe Judith Salvio Kapinga (wa kwanza kulia), na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, Mheshimiwa Prof. Riziki Silas Shemdoe, (wa kwanza kushoto) katika hafla ya uzinduzi wa soko jipya la Kariakoo Dar es Salaam uliofanyika tarehe 9 Februari, 2026 Jijini Dar es Salaam.*

**DODOMA** **MEI, 2026.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA JUDITH SALVIO KAPINGA (MB.), WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/2027

**DODOMA** **MEI, 2026**



**Mhe. Judith Salvio Kapinga (Mb.)**
**Waziri wa Viwanda na Biashara**



**Mhe. Dennis Lazaro Londo (Mb.)**
**Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara**



***Balozi* Waziri Rajab Salum**
**Katibu Mkuu wa Viwanda na Biashara**



**Aristides Robert Mbwasi**
**Naibu Katibu Mkuu wa Viwanda na Biashara**

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| **AfCFTA** | African Continental Free Trade Area |
| **BOT** | Bank of Tanzania |
| **BPRA** | Business and Property Registration Agency |
| **BRELA** | Business Registrations and Licensing Agency |
| **CAMARTEC** | Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology |
| **CBE** | College of Business Education |
| **CCM** | Chama Cha Mapinduzi |
| **CCTV** | Closed-circuit Television |
| **CEPA** | Comprehensive Economic Partnership Agreement |
| **CGS** | Credit Guarantee Scheme |
| **CIIE** | China International Import Expo |
| **CTI** | Confederation of Tanzania Industries |
| **DITF** | Dar es Salaam International Trade Fair |
| **Dkt** | Daktari |
| **DRC** | Democratic Republic of the Congo |
| **EAC** | East African Community |
| **eGA** | e- Government Authority |
| **EPA** | Economic Partnership Agreement |
| **EU** | European Union |
| **EWURA** | Energy and Water Utilities Regulatory Authority |
| **FCC** | Fair Competition Commission |
| **FCT** | Fair Competition Tribunal |
| **GCLA** | Government Chemist Laboratory Authority |
| **GCV** | Gross Calorific Value |
| **GNT** | Government Negotiation Team |
| **GP** | General Petroleum |
| **GTI** | Guided Trade Initiative |
| **ICDs** | Inland Container Depots |
| **IPAS** | Industrial Property Automation System |
| **ISO** | International Organization for Standardization |
| **JICA** | Japan International Cooperation Agency |
| **JTC** | Joint Trade Commission |
| **JWK** | Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo |
| **JWT** | Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania |

| | |
|---|---|
| **KMTC** | Kilimanjaro Machine Tools Company |
| **KOICA** | Korea International Cooperation Agency |
| **KOIMA** | Korea Importers Association |
| **LPG** | Liquefied Petroleum Gas |
| **Ltd** | Limited |
| **MSD** | Medical Stores Department |
| **MSMEs** | Micro, Small and Medium Enterprises |
| **NARCO** | National Ranching Company |
| **NBS** | National Bureau of Statistics |
| **NCTF** | National Committee on Trade Facilitation |
| **NDC** | National Development Corporation |
| **NEDF** | National Entrepreneurship Development Fund |
| **NIIMS** | National Industrial Information Management System |
| **NTBs** | Non Tarrif Barriers |
| **OC** | Other Charges |
| **ORS** | Online Registration System |
| **PBPA** | Petrorium Bulk Procurement Agency |
| **SADC** | Southern African Development Community |
| **SADCAS** | Southern African Development Community Accreditation Service |
| **SDIG** | Shudao Investment Group Company Limited |
| **SHG** | Sichuan Hongda Group Company Limited |
| **SHIMIWI** | Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali |
| **SHIMMUTA** | Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma Taasisi na Makampuni Binafsi |
| **SIDO** | Small Industries Development Organization |
| **SMEs** | Small and Medium Enterprises |
| **SIMSOPA** | Singida Municipal Sunflower Oil Processors Association |
| **STR** | Simplified Trade Regime |
| **TAMISEMI** | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **TANROADS** | Tanzania National Roads Agency |
| **TANTRADE** | Tanzania Trade Development Authority |
| **TBPL** | Tanzania Biotech Products Limited |
| **TBS** | Tanzania Bureau of Standards |

| | |
|---|---|
| **TCIAA** | Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture |
| **TCRA** | Tanzania Communications Regulatory Authority |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TEMDO** | Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization |
| **TFA** | Trade Facilitation Agreement |
| **TFRA** | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority |
| **TIN** | Taxpayer Identification Number |
| **TIRDO** | Tanzania Industrial Research and Development Organization |
| **TMDA** | Tanzania Medicines and Medical Devices Authority |
| **TNBC** | Tanzania National Business Council |
| **TNBP** | Tanzania National Business Portal |
| **TNCC** | Tanzania National Chambers of Commerce |
| **TPA** | Tanzania Port Authority |
| **TPC** | Tanganyika Planting Company |
| **TPI** | Tanzania Phamarcetical Industry |
| **TPSF** | Tanzania Private Sector Federation |
| **TRA** | Tanzania Revenue Authority |
| **TWCC** | Tanzania Women Chambers of Commerce |
| **UNCTAD** | United Nations Conference on Trade and Development |
| **UNIDO** | United Nations Industrial Development Organization |
| **USD** | United States Dollar |
| **VITEKI** | Vitovu vya Teknolojia za Kihandisi |
| **WMA** | Weights and Measures Agency |
| **WRRB** | Warehouse Receipts Regulatory Board |
| **WRS** | Warehouse Receipt System |
| **WTO** | World Trade Organization |
| **ZMA** | Zambia Metrology Agency |

*YALIYOMO*

**1. UTANGULIZI.................................................. 1**

**2. HALI NA MWENENDO WA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA NCHINI. 4**

2.1 VIWANDA .................................................. 4

*2.1.1 Hali ya Uzalishaji Viwandani .................................................. 5*

*2.1.2 Viwanda Vingine Vipya Vilivyojengwa .................................................. 12*

2.2 BIASHARA .................................................. 13

2.3 MCHANGO WA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA NCHINI .................................................. 19

**3. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026 ........ 20**

3.1 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026 .................................................. 21

*3.1.1 Fedha Zilizoidhinishwa na Kupokelewa .................................................. 21*

*3.1.2 Fedha za Matumizi ya Kawaida .................................................. 21*

*3.1.3 Fedha za Maendeleo .................................................. 22*

3.2 UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA 2025/26 .................................................. 22

*3.2.1 Maendeleo ya Viwanda .................................................. 22*

*3.2.2 Uendelezaji wa Jasiriamali Ndogo na za Kati .................................................. 33*

*3.2.3 Mtangamano wa Biashara .................................................. 35*

*3.2.4 Maendeleo ya Biashara .................................................. 46*

**4. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2026/2027 .................... 82**

4.1 VIPAUMBELE .................................................. 82

4.2 KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA NA WIZARA NA TAASISI .................................................. 83

*4.2.1 Sekta ya Maendeleo ya Viwanda .................................................. 84*

*4.2.2 Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo .................................................. 86*

*4.2.3 Sekta ya Biashara .................................................. 86*

**5. SHUKRANI .................................................. 92**

**6. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/2027 .................................................. 93**

## *ORODHA YA MAJEDWALI*

*JEDWALI NA. 1: ORODHA YA VIWANDA VYA KUBANGUA KOROSHO VITAKAVYO FANYA KAZI MSIMU WA 2026/2027* .......... 95
*JEDWALI NA.2: ORODHA YA VIWANDA VYA MBOLEA NCHINI* .......... 103
*JEDWALI NA. 3: MAUZO YA TANZANIA DUNIANI KUANZIA MWAKA 2021 HADI 2025 KWA DOLA ZA MAREKANI (USD MILIONI)* .......... 105
*JEDWALI NA. 4: MWENENDO WA BIASHARA BAINA YA TANZANI NA SOKO LA UMOJA WA ULAYA (EU) KWA MWAKA 2016 HADI 2025 KWA DOLA ZA MAREKANI (000`000)* .......... 105
*JEDWALI NA. 5 : BIASHARA YA BIDHAA KATI YA TANZANIA NA NCHI ZA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC) KWA MWAKA 2016 HADI 2025 (DOLA ZA MAREKANI "000,000")* ... 106
*JEDWALI NA. 6: BIASHARA KATI YA TANZANIA NA JUMUIYA YA MAENDELEO YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC) KWA MWAKA 2016 HADI 2025 (DOLA ZA MAREKANI '000,000')* .......... 106
*JEDWALI NA. 7: MWENENDO WA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA BARA LA ASIA KUANZIA MWAKA 2019 HADI 2025 KWA DOLA ZA MAREKANI (000`000)* .......... 106
*JEDWALI NA. 8: MWENENDO WA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA CHINA KUANZIA MWAKA 2020 HADI 2025 KWA DOLA ZA MAREKANI (000'000)* .......... 107
*JEDWALI NA. 9: MWENENDO WA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA INDIA KUANZIA MWAKA 2020 HADI 2025 KWA DOLA ZA MAREKANI (000'000)* .......... 107
*JEDWALI NA. 10: MWENENDO WA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA JAPAN KUANZIA MWAKA 2020 HADI 2025 KWA DOLA ZA MAREKANI (000'000)* .......... 107
*JEDWALI NA. 11: MWENENDO WA MCHANGO WA SEKTA YA VIWANDA KATIKA PATO LA TAIFA 2019 - 2025* .......... 107
*JEDWALI NA. 12: UKUAJI WA SEKTA YA VIWANDA 2019 - 2025* .......... 107
*JEDWALI NA. 13: MWENENDO WA MCHANGO WA SEKTA YA BIASHARA KATIKA PATO LA TAIFA 2019 - 2025* .......... 107
*JEDWALI NA. 14: UKUAJI WA SEKTA YA BIASHARA 2019 - 2025* .......... 108
*JEDWALI NA. 15: MAOMBI YA MIKOPO YALIYOPOKELEWA NA KUTOLEWA KUANZIA JULAI, 2025 HADI APRILI, 2026* .......... 108
*JEDWAA NA. 16: ASILIMIA YA MAREJESHO YA MIKOPO KUANZIA JULAI, 1994 HADI MACHI, 2025* .......... 109
*JEDWALI NA. 17: MCHANGANUO WA MAENEO YALIYOTENGWA* .......... 110
*JEDWALI NA. 18: UZITO WA BIDHAA ZILIZOUZWA KUPITIA WRS HADI APRILI, 2026* .......... 110

## 1. UTANGULIZI

***1. Mheshimiwa Spika;*** kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara tarehe 24 na 26 Machi, 2026, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2025/2026. Aidha, ninaliomba Bunge lako likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2026/2027.

***2. Mheshimiwa Spika;*** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa afya njema na kuwepo hapa siku hii muhimu ya leo.

***3. Mheshimiwa Spika;*** kwa unyenyekevu na moyo wa shukrani, nitumie nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Kupitia bunge hili tukufu nimuahidi Mheshimiwa Rais kushirikiana na watendaji wenzangu akiwemo Naibu Waziri, Watumishi wa Wizara na Taasisi pamoja na wadau wote wa Wizara katika kutekeleza majukumu aliyonikabidhi na kufuata miongozo anayonipatia ili tuweze kufikia malengo mahsusi ya kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara.

***4. Mheshimiwa Spika;*** naomba nitumie tena fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania wa Awamu ya Sita. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Balozi Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Viongozi hawa wamekuwa wakitoa miongozo na maelekezo mbalimbali ambayo yamesaidia sana katika kutekeleza majukumu ya Sekta ya Viwanda na Biashara. Nawashukuru sana.

***5. Mheshimiwa Spika;*** napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kipindi kingine. Hii ni kutokana na utendaji wake mzuri ambao umewapa wananchi wa Zanzibar imani juu yake.

***6. Mheshimiwa Spika;*** ninapenda kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa umakini na umahiri wenu katika kuliongoza na kulisimamia Bunge letu. Halikadhalika, nawapongeza watoa hoja wote waliowasilisha hotuba zao kabla yangu. Kipekee nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Hotuba yake ya Bajeti aliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 1 Aprili, 2026. Hotuba hiyo inatoa hali ya utekelezaji wa jumla katika utendaji wa Serikali kwa Mwaka 2025/2026 pamoja na kuonesha dira na mwelekeo wa Taifa letu kwa Mwaka 2026/2027 katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya Viwanda na Biashara.

***7. Mheshimiwa Spika***; katika mwaka 2025/2026 Bunge lako Tukufu liliondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge,Uratibu na Wenye Ulemavu) na

Mbunge wa Jimbo la Ismani; Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Naomba nitoe pole kwako Mheshimiwa Spika; Waheshimiwa Wabunge wote; familia; ndugu na jamaa; na wananchi.Tunaomba mwenyezi Mungu aendelee kuwapa pumziko la milele.

***8. Mheshimiwa Spika;*** kwa dhati kabisa naomba kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Mbunge wa Kondoa Mjini. Kamati hii imekuwa na mchango Madhubuti kwa Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake kupitia maelekezo, maoni na ushauri katika masuala mbalimbali hususan maendeleo ya viwanda na biashara nchini.

***9. Mheshimiwa Spika;*** kwa moyo wa shukrani namshukuru Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Naibu Waziri na Mbunge wa Mikumi kwa umadhubuti wake na kwa mchango mkubwa anaoutoa katika Wizara yetu. Naibu Waziri ni kiongozi mchapakazi, anayejituma na anayependa kazi yake. Namshukuru, Mheshimiwa Balozi Waziri Rajab Salum, Katibu Mkuu kwa utendaji wake mahiri, Bw. Aristides Robert Mbwasi, Naibu Katibu Mkuu, viongozi wa Bodi, watendaji na watumishi wote wa Wizara na taasisi zote 13 zilizo chini ya Wizara, pamoja na wasaidizi wa ofisi yangu, katibu wangu Bi. Loyce Lubonera, Dereva wangu, Bw. Paul Mtulo na Mwandishi Mwendesha Ofisi yangu, Bi. Pheby Bundala. Nawashukuru kwa utumishi wao.

***10.Mheshimiwa Spika;*** ninapohitimisha salamu za awali na

za shukrani, naomba niishukuru familia yangu, Mume Wangu kwa namna anavyonipa utulivu unaonisaidia katika kutimiza majukumu yangu. Namshukuru sana yeye, Watoto wetu na wazazi wangu kwa namna wanavyoniwezesha kufanya majukumu yangu kwa ufanisi. Mwisho kwa hatua hii, nawashukuru sana, wananchi wenzangu wa Jimbo la Mbinga Vijijini, kwa kunipa kura za heshima za kuwa Mbunge wa kwanza mwanamke wa Jimbo letu. Nawaahidi kuwatumikia kwa upendo  na moyo thabiti.

***11.Mheshimiwa Spika;*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kipindi cha mwaka 2025/2026 na mpango wa mwaka 2026/2027.

## 2. HALI NA MWENENDO WA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA NCHINI

### 2.1 Viwanda

***12.Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya biashara ili kuchochea mageuzi ya uchumi fungamanishi, jumuishi na shindani unaojengwa katika msingi wa kuongeza thamani ya rasilimali zinazozalishwa nchini na kuimarisha viwanda vinavyozalisha bidhaa kwa wingi kwa kutumia malighafi za ndani. Jitihada hizo ni utekelezaji wa malengo ya Dira 2025 ambayo yamejielekeza katika kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa muhimu, kuzalisha bidhaa bora, kutoa ajira kwa wingi na kuongeza mauzo nje ya nchi. Kupitia mwelekeo huo, viwanda vipya vimejengwa na vingine vimefanyiwa upanuzi.

***13.Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha mwaka 2025/2026 jumla ya viwanda vipya vikubwa na vya kati 25 katika sekta mbalimbali vimejengwa na kuanza uzalishaji. Viwanda hivyo vimetoa jumla ya ajira 39,250 ambapo ajira za moja kwa moja ni 7,635 na zisizo za moja kwa moja ni 31,615.

### *2.1.1 Hali ya Uzalishaji Viwandani*

***14.Mheshimiwa Spika;*** hali ya uzalishaji viwandani imeendelea kuimarika na kutoa mchango mkubwa katika uchumi. Naomba uniruhusu nielezee kuhusu baadhi ya viwanda vinavyozalisha bidhaa muhimu zinazotumika kwa wingi nchini na vyenye uwekezaji mkubwa.

### *A. Viwanda vya Mabati*

***15.Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina viwanda vikubwa vitano (5) vya mabati ambavyo ni Lodhia, MMI Steel, ALAF Limited, Kinglion na GSM Roofing Sheet ambavyo vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha mabati tani 410,000 ya rangi na tani 700,000 meupe kwa mwaka. Hadi kufikia Aprili, 2026, viwanda hivyo vimezalisha jumla ya tani 350,000 za mabati ya rangi na tani 500,000 ya mabati meupe sawa na asilimia 70 ya uzalishaji wa mabati nchini. Aidha, mahitaji ya mabati ya rangi ni takriban tani 250,000 na mabati meupe ni 380,000. Mabati ya ziada huuzwa katika nchi za Burundi, Rwanda, DRC na Malawi. Viwanda hivyo vimetoa ajira za moja kwa moja 2,300 na zisizo za moja kwa moja 11,500.

***16.Mheshimiwa Spika;*** kati ya viwanda hivyo vikubwa, kiwanda cha GSM Roofing Sheet kilichopo Dar es salaam ni kipya na kinazalisha mabati ya rangi chenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha mabati tani 150,000 kwa mwaka na kutoa ajira za moja kwa moja 800 na zisizo za moja kwa moja 3,000. Hadi kufikia Aprili, 2026 kiwanda kimezalisha mabati tani 45,000. Pamoja na kukidhi uzalishaji kwa ajili ya matumizi

ya ndani ya mabati, Wizara kupitia NDC, inatekeleza mkakati wa kuongeza uzalishaji wa mabati na kupunguza uagizaji wa malighafi kutoka nje ya nchi kwa kusaini mkataba wa mradi wa Maganga Matitu na kampuni ya Fijuan Hexingwang Industry Tanzania Co. Ltd. Mradi huu unakadiriwa kuwa na hifadhi ya chuma tani milioni 101. Hatua iliyofikiwa ni uingizaji wa mitambo ya uchimbaji na uchakataji wa madini ya chuma. Pindi mradi huo utakapoanza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali za chuma, utawezesha uanzishwaji wa viwanda vingine vitakavyoongeza mnyororo wa thamani (*downstream processing industries*).

## B. Viwanda vya Saruji

***17.Mheshimiwa Spika****;* Tanzania ina jumla ya viwanda 15 vya kuzalisha saruji vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 13,600,000 za saruji kwa mwaka. Kati ya hivyo, viwanda saba (7) vinazalisha clinker na saruji na viwanda nane (8) vinazalisha saruji pekee. Hadi kufikia Aprili, 2026, viwanda vimezalisha jumla ya tani 10,300,000 za saruji ambapo mahitaji ya sasa ni takribani tani 8,500,000 kwa mwaka. Saruji ya ziada huuzwa katika nchi mbalimbali zikiwemo Malawi, Zambia, DRC, Rwanda na Burundi. Viwanda hivyo vimetoa ajira za moja kwa moja 6,020 na zisizo za moja kwa moja 20,280. Ili kuongeza uzalishaji wa saruji nchini, katika mwaka 2025/2026 kiwanda kimoja (1) kinachozalisha saruji kimejengwa. Kiwanda hicho ni WIH holding Limited kilichopo Mkoa wa Kigoma ambacho kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 1,900,000 za saruji kwa mwaka na kutoa ajira za moja kwa moja 800 na zisizo za moja kwa moja 3,050. Hadi kufikia Aprili, 2026 kiwanda cha WIH Holding Limited kimezalisha saruji tani 1,500,000.

## C. Viwanda vya Sukari

***18.Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda saba (7) vya kuzalisha sukari ambavyo ni Kilombero Sugar Company Limited, Tanganyika Planting Company Limited (TPC - Kilimanjaro), Kagera Sugar Limited (Kagera), Mtibwa Sugar Estates Limited (Morogoro), Mkulazi Holding Company Limited (Morogoro), Manyara Sugar Limited (Manyara) na Bagamoyo Sugar Limited (Pwani). Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha sukari tani 800,000 kwa mwaka. Hadi kufikia Aprili, 2026, viwanda vimezalisha jumla ya tani 410,979 za sukari ambapo mahitaji ya sukari ni takriban 550,000. Aidha, viwanda hivyo vimetoa ajira za moja kwa moja 28,500 na zisizo za moja kwa moja 95,000.

***19.Mheshimiwa Spika;*** katika kuhakikisha nchi inapunguza uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi, viwanda viwili (2) vya Mkulazi Holding Company Limited na Kilombero Sugar Company Limited vimefanya upanuzi ili kuongeza uzalishaji wa sukari nchini. Kufuatia upanuzi huo, Kiwanda cha Kilombero kitakuwa na uwezo wa kuzalisha sukari tani 226,000 kutoka tani 123,000 kwa mwaka ambapo majaribio ya uzalishaji yamekamilika na uzalishaji utaanza mwezi Juni, 2026. Aidha, Kiwanda cha Mkulazi kimeongeza mtambo utakaowezesha kuzalisha sukari ya kiwandani (Industrial sugar). Majaribio ya mitambo yamefanyika na tayari kiwanda kimezalisha tani 256 za sukari ya kiwandani. Kukamilika kwa upanuzi huo, kunawezesha viwanda vyote viwili kuzalisha ajira za moja kwa moja 8,500 na zisizo za moja kwa moja 25,000.

## D. Viwanda vya Kubangua Korosho

***20.Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda 70 vya kubangua korosho ambapo kati ya viwanda hivyo, viwanda 50 vinafanya kazi, vinne (4) vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi na viwanda 16 havifanyi kazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uchakavu wa mitambo na teknolojia kupitwa na wakati. Viwanda vinavyofanya kazi vina uwezo uliosimikwa wa kubangua korosho jumla ya tani 108,549 kwa mwaka na kutoa ajira za moja kwa moja 6,900 na zisizo za moja kwa moja 18,000 **(Jedwali Na.1).** Hadi kufikia Aprili, 2026, viwanda hivyo vimebangua jumla ya tani 53,125 za korosho ambazo sawa na asilimia 8.6 ya uzalishaji wa korosho ghafi nchini ambapo kwa mwaka 2025/2026 uzalishaji ulikuwa tani 617,680.

***21.Mheshimiwa Spika;*** katika jitihada za kuongeza ubanguaji wa korosho nchini, jumla ya viwanda sita (6) vya kubangua korosho vimejengwa mwaka 2025/2026 ambavyo ni Work Point LTD; Ares Trading co.Ltd; Er-Kang (T) Co.Ltd; Sis International ltd; HK International Ltd; na ECO Broom Enterprises ambavyo vipo katika Mkoa wa Mtwara na Lindi. Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa wa kubangua korosho tani 11,400 kwa mwaka na kutoa ajira za moja kwa moja 210 na zisizo za moja kwa moja 605. Aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha wawekezaji kujenga viwanda vya kubangua korosho katika mikoa inayozalisha zao hili. Vilevile, katika kuunga juhudi hizo, Wizara kupitia CAMARTEC imejenga kiwanda darasa cha kubangua korosho katika Wilaya ya Manyoni katika Mkoa wa Singida kwa ajili ya kutoa mafunzo na utaalam wa kubangua korosho.

***22.Mheshimiwa Spika;*** pamoja na ujenzi wa viwanda hivyo, uhamasishaji wa ujenzi wa viwanda unaendelea ambapo jumla ya viwanda vinne (4) vinaendelea kujengwa katika Mkoa wa Mtwara ili kupunguza uuzaji wa korosho ghafi nje ya nchi. Viwanda hivyo ni kiwanda cha Grand Ruby Group Ltd; MATEAK Holdings Ltd; Tanzania Premium Cashews Ltd; na Akros Cashew Factory. Pindi viwanda vitakapokamilika, vitakuwa na uwezo wa kubangua korosho ghafi tani 153,600 kwa mwaka.

**E. Viwanda vya Mbolea**

***23.Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda 49 vya kuzalisha mbolea ambapo vikubwa ni viwili (2), vya kati ni 10 na vidogo ni 37 **(Jedwali Na. 2).** Viwanda vikubwa ni Minjingu na Itracom Fertilizer Limited na viwanda vya kati ni YARA Tanzania, ETG Inputs. Ltd, Tanga Mining Co. Ltd, Neelkanth Chemical Ltd, ABM Equipments Ltd, HSSL Lime Co. Ltd, Lavan Investment Limited, Dodoma Cement Co.ltd, Fert Pro Ltd pamoja na Tanzania Biotech Products Ltd (TBPL). Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 1,793,849 za mbolea kwa mwaka. Hadi kufikia Aprili, 2026, viwanda vimezalisha jumla ya tani 123,203 za mbolea na kutoa ajira za moja kwa moja 2,687 na zisizo za moja kwa moja 9,200.

***24.Mheshimiwa Spika;*** katika kupunguza uagizaji wa mbolea kutoka nje hususan mbolea ya chumvichumvi ambayo pia hutumika malighafi muhimu katika uzalishaji wa mbolea nyingine hapa nchini, Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta mwekezaji mahiri atakayeweza kutumia gesi asilia kuzalisha mbolea hiyo

## F. Viwanda vya Dawa za Binadamu na Vifaa Tiba

***25.Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina viwanda 14 vya kuzalisha dawa za binadamu na vifaa tiba ambavyo ni Zenufa Laboratories (T) Limited; Shelys Pharmaceuticals Limited; Prince Pharmaceuticals Ltd; Kairuki Pharmaceuticals Industry Ltd; Mansoor Daya Chemical Industries; Keko Pharmaceuticals (1997) Limited; Alfa Pharmaceuticals Limited; Katwaza Pharmaceuticals Industry Ltd; A.A Pharmaceuticals Ltd; Sri Balaj Pharmaceuticals Ltd; Bhanji Pharmaceuticals Ltd; Cure Afya Pharmaceuticals Limited; Tanzania Pharmaceutical Industries (TPI) ARV Ltd; na ER-KANG Tanzania. Viwanda hivyo vina uwezo wa kuzalisha asilimia 20 ya dawa na vifaa tiba zinazohitajika hapa nchini. Katika kukabiliana na uagizaji wa dawa kutoka nje ya nchi, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mahsusi ili kuhakikisha sekta hii inaongeza uwekezaji wa viwanda vya dawa na vifaa tiba angalau kufikia asilimia 60 ya mahitaji ya dawa na vifaa tiba ifikapo 2035.

***26.Mheshimiwa Spika:*** katika mwaka 2025/2026 jumla ya viwanda 11 vimejengwa na kuanza majaribio ya uzalishaji wa dawa za binadamu na vifaa tiba. Kati ya viwanda hivyo, viwanda viwili (2) vinazalisha maji tiba, viwanda vitatu (3) vitendanishi vya maabara, viwanda vitatu (3) dawa za vidonge na maji na viwanda vitatu (3) vinazalisha vifaa tiba. Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha vizio (units) bilioni 3.5 za dawa za binadamu na kutoa ajira za moja kwa moja 4,200 na zisizo za moja kwa moja 21,000. Hadi kufikia Aprili, 2026 viwanda hivyo vimezalisha vizio (units) bilioni 1.2 za dawa za binadamu. Aidha, kiwanda cha kuzalisha dawa za kufubaza virusi vya ukimwi (ARV) cha Tanzania Pharmaceutical Industries (TPI) kilichopo Arusha kimeanza ukarabati ikiwa ni juhudi za kuzalisha dawa hizi hapa nchini.

## G. Viwanda vya Mafuta ya Kula

***27.Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda 1,604 vya kuzalisha mafuta ya kula ambapo 1,038 ni vidogo sana, 543 vidogo, tisa (9) vya kati na 14 vikubwa. Viwanda hivi vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha mafuta ya kula tani 2,527,739 kwa mwaka na vimetoa ajira za moja kwa moja 10,755 na zisizo za moja kwa moja 36,416. Aidha, viwanda hivyo vinazalisha tani 302,000 za mafuta ambapo mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni takriban tani 700,000 kwa mwaka. Hivyo tani 430,000 huagizwa ili kutosheleza mahitaji ya ndani.

***28.Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeendelea na juhudi mbalimbali za nchi kujitosheleza na mahitaji ya mafuta ya kula. Juhudi hizo zinajumuhisha kuzalisha mbegu bora na kuzigawa kwa wakulima; kutoa ruzuku ya mbolea; kuendelea kuhamasisha wawekezaji wakubwa kuwekeza katika uzalishaji wa mbegu za mafuta ya kula; na kuendelea kuboresha teknolojia za wasindikaji wadogo.

***29.Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2025/2026, kiwanda cha Vion Win Ltd cha kukamua na kusafisha mafuta ya kula ya alizeti pamoja na kuzalisha mashudu kwa ajili ya chakula cha mifugo kilichopo Mkoa wa Singida kimejengwa. Kiwanda hicho kimewekeza mtaji wa takriban shilingi bilioni 5.5. Hadi kufikia Aprili, 2026, kiwanda kimetoa ajira za moja kwa moja 70 na zisizo za moja kwa moja 300. Kiwanda kina uwezo uliosimikwa wa kuchakata tani 100 za mbegu za alizeti kwa siku. Aidha, kiwanda cha Mainland Group Agro Process Co. Ltd kilichopo Dodoma kimefanya upanuzi utakaowezesha kiwanda kusindika mbegu za alizeti kiasi cha tani 150,000 kutoka tani 75,000 kwa mwaka. Hadi kufikia Aprili, 2026 kiwanda kimezalisha mafuta ya kula tani 48,000 na kutoa ajira za moja kwa moja 450 na zisizo za moja kwa moja 2,000.

### *2.1.2 Viwanda Vingine Vipya Vilivyojengwa*

***30.Mheshimiwa Spika;*** *v*iwanda vipya vilivyojengwa katika sekta ndogo nyingine ni vifuatavyo:

***a) Kiwanda cha Afriport Apparel***

***31.Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha *Afriport Apparel* kilichopo jijini Dar es Salaam ni uwekezaji wa kimkakati unaozalisha nguo maalum za kujikinga mahala pa kazi (protective gears). Kiwanda kimewekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 8.8 na kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha jozi milioni 10 za mavazi kwa mwaka na kutoa ajira za moja kwa moja 1,000 na ajira zisizo za moja kwa moja 2,500. Kiwanda kilianza uzalishaji mwezi Februari, 2026 na hadi kufikia Aprili, 2026 kimezalisha jozi 50,000 za mavazi na kutoa ajira za moja kwa moja 200 na zisizo za moja kwa moja 600.

***b) Kiwanda cha Giant Group Co. Ltd***

***32.Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha Giant Group Co. Ltd kipo Mkoa wa Pwani na kinazalisha nyaya na vifaa vya umeme. Kiwanda kimewekeza mtaji wa takriban dola za Marekani milioni 15 na kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha nyaya za umeme tani 4 kwa siku. Hadi kufikia Aprili, 2026, kimezalisha tani 520 na kutoa ajira za moja kwa moja 120 na zisizo za moja kwa moja 250.

***c) Kiwanda cha Magodoro cha Federal***

***33.Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha Federal kilichopo Mkuranga, Mkoa wa Pwani, kinazalisha magodoro ya sponji (foam), mito na bidhaa nyingine za malazi. Kiwanda kimewekeza mtaji wa shilingi bilioni 8.7 na kina uwezo wa kuzalisha wastani wa magodoro 1,000 kwa siku. Hadi kufikia Aprili, 2026, kiwanda kimezalisha magodoro 8,000 na kutoa ajira za moja kwa moja 140 na zisizo za moja kwa moja 350.

### d) Kiwanda cha Dawa za Mifugo cha FarmBase

**34.*Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha FarmBase kilichopo Kigamboni, Dar es Salaam, kinajishughulisha na utengenezaji wa dawa za mifugo na virutubisho. Kiwanda kimewekeza mtaji wa shilingi bilioni 10.2 na kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha dawa za mifugo za maji na unga tani 200,000 kwa mwaka. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya tani 152.7 za dawa za maji na unga zimezalishwa na kutoa ajira za moja kwa moja 95 na zisizo za moja kwa moja 200. Bidhaa hizo huuzwa nchini na katika nchi za Zambia na Malawi.

### e) Kiwanda cha Starlink Gulf Trading Ltd

**35.*Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha Starlink Gulf Trading Ltd kilichopo Bagamoyo Mkoa wa Pwani, kinazalisha chokaa (white skim wallputty) na kimewekeza mtaji wa shilingi bilioni 15 kikiwa na uwezo wa kuzalisha wastani wa chokaa tani 900 kwa siku. Hadi kufikia Aprili, 2026, kiwanda kimezalisha tani 113,400 na kutoa ajira za moja kwa moja 200 na zisizo za moja kwa moja 360. Bidhaa hizo huuzwa nchini na katika nchi za DRC, Burundi, Zambia na Malawi.

## 2.2 Biashara

### A. Hali ya Biashara Duniani

**36.*Mheshimiwa Spika;*** biashara ya Tanzania nje ya nchi imekuwa ikiongozeka mwaka hadi mwaka. Mathalan thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 10,080.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 8,702.0 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 16. Ongezeko hilo linatokana na kuimarika kwa mikakati ya kuboresha mazingira ya biashara

nchini, utafutaji wa masoko, kuzalisha bidhaa zinazokidhi ushindani nje ya nchi na kupunguza milolongo ya hatua za kusafirisha bidhaa nje ya nchi. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na mazao ghafi ya kilimo kama; ufuta, tumbaku, mbaazi, ngano, mchele maharage, mahindi, kahawa, pamba na parachichi; Mazao ghafi ya Mifugo ni pamoja na, samaki na bidhaa za viwandani ikiwa ni pamoja na dhahabu, kakao, makaa ya mawe, vigae, na mabati.

***37.Mheshimiwa Spika;*** mwaka 2025, bidhaa zilizoingizwa nchini zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 16,031.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 15,684.5 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 2.2. Ongezeko hilo linatokana na kuagiza kwa wingi bidhaa ambazo hazizalishwi hapa nchini na zinazotumia teknolojia ya juu. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni pamoja na bidhaa za mitaji (Capital goods), magari, bidhaa za kutengeneza lami, bidhaa za chuma, mashine mbalimbali za hospitalini, madawa baridi, mafuta ya petroli na gesi na sukari ya viwandani **(Jedwali Na.3)**.

**B. Soko la Umoja wa Ulaya (EU)**

***38.Mheshimiwa Spika;*** mwaka 2025, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda nchi za Umoja wa Ulaya yameongezeka kufikia dola za Marekani milioni 943.8 kutoka dola za Marekani milioni 686.3 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 37.5. Ongezeko hilo limetokana na kuimarika kwa ushiriki wa wafanyabiashara wa Tanzania katika soko hilo, juhudi za Serikali na sekta binafsi katika kuboresha ubora wa bidhaa ili kukidhi viwango vya soko la Umoja wa Ulaya na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za kikaboni (organic products). Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na maharage, tumbaku, samaki, parachichi, kahawa,

kakao, asali, mafuta ya alizeti, madini, chai, maua, matunda, pamba, mbogamboga, ngozi na vito vya thamani.

***39.Mheshimiwa Spika;*** kwa mwaka 2025, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za Umoja wa Ulaya ilikuwa dola za Marekani milioni 1,260.13 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,267.6 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 0.6. Upungufu huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani wa baadhi ya bidhaa kama vile mafuta ya kula, bidhaa za plastiki na vifaa vya msingi viwandani. Bidhaa zinazoagizwa kwa wingi kutoka Umoja wa Ulaya ni pamoja na mashine na mitambo inayotumiwa viwandani, vifaa vya usafiri, kemikali, dawa za binadamu, vifaa vya umeme, mbolea, plastiki na bidhaa zake **(Jedwali Na.4)**.

## C. Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)

***40.Mheshimiwa Spika;*** mwaka 2025 Tanzania iliuza bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 1,264.6 katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ikilinganishwa na dola za Marekani Milioni 1,163.8 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 8.7. Ongezeko hilo limechangiwa na juhudi za serikali za kuboresha mazingira ya biashara nchini na kuimarika kwa uzalishaji wa bidhaa ambazo zina soko kubwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni vitunguu, samaki, karanga, nyanya, asali, maharage, mbaazi, dagaa, mahindi, ngano, mchele, karatasi, mabati na vigae.

***41.Mheshimiwa Spika;*** mwaka 2025 bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 563.1 ziliagizwa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 527.3 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.8. Ongezeko hilo limetokana na

kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani nchini na kupelekea kuongeza manunuzi ya bidhaa za Viwandani kutoka nchi za jirani ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni sabuni za kuogea, vifaa vya mitaji, vyakula vilivyosindikwa, misumari, dawa za viatu, maziwa na vifaa vya usafirishaji **(Jedwali Na.5)**.

## D. Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

***42.Mheshimiwa Spika;*** mwaka 2025 thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ilikuwa dola za Marekani milioni 3,545.0 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,968.0 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 19.4. Ongezeko hilo limechangiwa na mauzo ya bidhaa kama vile madini, samaki, nyanya, vitunguu, maharage, viazi vitamu, ndizi, nanasi, parachichi, machungwa, majani ya chai, mchele, kahawa, vyandarua, saruji, sabuni na mafuta ya kupaka.

***43.Mheshimiwa Spika;*** bidhaa zilizoagizwa kutoka Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 837.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 786.4 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.6. Bidhaa zilizoagizwa ni pamoja na pombe aina ya *whisky,* mbegu za alizeti, vifaa vya usafi, meza za mbao, magari, kemikali, na juisi mchanganyiko **(Jedwali Na. 6)**.

## E. Bara la Asia

***44.Mheshimiwa Spika:*** mwaka 2025, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda baadhi ya nchi za Bara la Asia tunazofanya biashara kwa wingi husussan kwa nchi za China, India na

Japan ilikuwa dola za Marekani milioni 3,213.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,840.3 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 13.1(Jedwali Na. 5). Ongezeko hilo lilichangiwa na uhitaji mkubwa wa bidhaa kama vile ufuta, kakao na parachichi. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na madini, mazao jamii ya kunde, korosho, parachichi, pamba, tumbaku, ufuta, kakao na samaki.

***45.Mheshimiwa Spika:*** uagizaji wa bidhaa kutoka baadhi ya nchi za Bara la Asia ulikuwa na thamani dola za Marekani milioni 10,093 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,514.2 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 83. Ongezeko hilo limechangiwa na uhitaji mkubwa wa bidhaa na huduma katika Sekta ya Usafirishaji na Uchukuzi. Bidhaa zilizonunuliwa kwa wingi ni pamoja na magari; pikipiki; mafuta ya gesi na petrol; bidhaa za chuma; dawa na vifaa tiba; matairi; na mabehewa ya treni **(Jedwali Na. 7)**.

***i. China***

***46.Mheshimiwa Spika;*** katika nchi ya China, Tanzania inanufaika na msamaha wa malipo ya ushuru wa forodha kwa asilimia 98 ya bidhaa zote zinazouzwa kwenye soko la China. Mwaka 2025 mauzo ya Tanzania kwenda nchini China yalikuwa dola za Marekani milioni 512.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 442.96 mwaka 2024 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 15.7. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi China zilikuwa ni madini na makinikia, minofu ya samaki, mbegu za ufuta, tumbaku, mafuta ya ufuta, pamba na kahawa.

***47.Mheshimiwa Spika;*** uagizaji uliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 5,643.3 mwaka 2025 kutoka dola za Marekani milioni 4,780.15 mwaka 2024 sawa na ongezeko la

asilimia 18.1. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni pamoja na zana za kilimo; pikipiki za miguu miwili na mitatu; mashine na mitambo; bidhaa za chuma; rola za mabati; transfoma; magari na bomba (**Jedwali Na.8**).

### *ii. India*

***48.Mheshimiwa Spika;*** mwaka 2025 mauzo ya Tanzania kwenda India yalikuwa dola za Marekani milioni 938.03 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,637.03 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 42.7. Upungufu huo umechangiwa na kushuka kwa mauzo ya bidhaa za korosho, madini (dhahabu na shaba) na pamba ambazo ziliuzwa kwenye masoko mengine kama vile China. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni korosho; mbaazi; dhahabu; njegere; pamba; na parachichi.

***49.Mheshimiwa Spika;*** mwaka 2025 bidhaa zilizoagizwa kutoka India zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 2,041.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,130.65 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 4.2. Upungufu huo ulitokana na bidhaa kama vile pikipiki kupatikana katika masoko mengine kama vile China. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni pamoja na mafuta ya petroli; dawa na vifaa tiba; vifaa vya ujenzi; mapazia; pikipiki za miguu miwili na mitatu; na sukari nyeupe (**Jedwali Na. 9**).

### *iii. Japan*

***50.Mheshimiwa Spika;*** kwa upande wa Japan, mwaka 2025 mauzo ya Tanzania kwenda Japan yalikuwa dola za Marekani milioni 110.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 99.82 mwaka 2024 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 10.8. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamba, kakao, samaki, ufuta, pareto na bidhaa za mkonge na nyuzi.

**51.Mheshimiwa Spika;** thamani ya bidhaa zilizoagizwa iliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 692.4 mwaka 2025 kutoka dola za Marekani milioni 593.2 mwaka 2024 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 16.7. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni pamoja na magari, vifaa vya magari, mitambo, rola ya mabati, baiskeli, matairi ya magari na machine mbalimbali (**Jedwali Na.10**).

## *2.3 Mchango wa Sekta ya Viwanda na Biashara Nchini*

***52.Mheshimiwa Spika;*** Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa kwa mwaka 2025 ulikuwa asilimia 5.9 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2024 **(Jedwali Na. 11).** Pamoja na kushuka kwa mchango wa sekta katika Pato la Taifa, Sekta ya viwanda imeendelea kukua ambapo katika mwaka 2025 imekuwa kwa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2024 **(Jedwali Na.12).**

***53.Mheshimiwa Spika;*** Mchango wa Sekta ya Biashara katika Pato la Taifa kwa mwaka 2025 umeendelea kuwa asilimia 8.6 sawa na mwaka 2024 **(Jedwali Na. 13)**. Aidha, kasi ya ukuaji wa Sekta ya Biashara ilikuwa asilimia 5.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2024. Ukuaji huo umechangiwa na uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara **(Jedwali Na. 14)**.

## *2.4 Sera Zilizofanyiwa Marejeo*

***54.Mheshimiwa Spika;*** katika kuboresha mazingira ya ujenzi wa viwanda na ufanyaji biashara, Wizara katika mwaka 2025/2026 imekamilisha mapitio ya sera mbili (2) ambazo ni Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Mwaka 1996-2020 ambayo kwa sasa inajulikana kama Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 2025; na Sera ya Maendeleo

ya Viwanda Vidogo na Biashara ya Mwaka 2003 ambayo kwa sasa inajulikana kama Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya Mwaka 2003 (Toleo la Mwaka 2025).

***55.Mheshimiwa Spika;*** Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 2025 ina lenga kuimarisha uongezaji thamani na mnyororo wa thamani katika mazao na rasilimali nyingine; kuanzisha na kuimarisha viwanda vya kimkakati; kuwezesha upatikanaji na ufikiwaji wa masoko ya bidhaa za ndani na nje ya nchi; kuwezesha utafiti na ubunifu wa teknolojia za viwanda; na kujumuisha masuala mtambuka katika maendeleo ya viwanda. Aidha, Sera inayosimamia wajasiriamali inalenga kuimarisha miundombinu wezeshi ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati; kuimarisha ukuaji wa jasiriamali; kuongeza matumizi ya teknolojia na ubunifu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati; kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati; kuwezesha upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo na wa kati; na kujumuisha masuala mtambuka katika shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati.

## 3. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026

***56.Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2025/2026, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ilani ya CCM, Mpango Mkakati wa Wizara, Mipango mingine ya Kitaifa, maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Itifaki na makubaliano ya kikanda na kimataifa. Vilevile, Wizara imetekeleza maeneo ya kipaumbele yakiwemo kuwezesha uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda na biashara nchini; na kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati ya Liganga na Mchuchuma na Magadi soda Engaruka.

***57.Mheshimiwa Spika;*** maeneo mengine ni kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma kwa kuboresha mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya mitaa ya viwanda (Industrial Clusters) kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati; kuboresha mazingira ya biashara na kuchochea ukuaji wa sekta binafsi; kuendelea na utafutaji wa masoko kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini; kuimarisha usimamizi wa ubora na usalama wa bidhaa nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vipodozi; na kuratibu majadiliano baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa.

## *3.1 Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2025/2026*

### *3.1.1*Fedha Zilizoidhinishwa na Kupokelewa

***58.Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2025/2026 Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Fungu 44 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 135,788,232,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 93,900,697,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 41,887,535,000.00 ni za miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara ilipokea shilingi 95,630,301,245.82 sawa na asilimia 70.43 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 74,603,022,813.73 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 21,027,278,432.09 ni za miradi ya maendeleo.

### *3.1.2Fedha za Matumizi ya Kawaida*

***59.Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2025/2026 Wizara iliidhinishiwa shilingi 93,900,697,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 18,081,317,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na shilingi 75,819,380,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara ilipokea jumla ya shilingi

74,603,022,813.73, sawa na asilimia 79.45 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 14,336,465,376.94 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), na shilingi 60,266,651,284.37 kwa ajili ya Mishahara.

#### *3.1.3Fedha za Maendeleo*

***60.Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2025/2026 Wizara iliidhinishiwa shilingi 41,887,535,000.00 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 27,870,710,000 ni fedha za ndani na shilingi 14,016,825,000 ni fedha za nje. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara ilipokea shilingi 21,027,278,432.09 sawa na asilimia 75.45 ya bajeti ya fedha za ndani za maendeleo.

### *3.2 Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2025/2026*

#### *3.2.1*Maendeleo ya Viwanda

#### *A. Kuendeleza Miradi ya Kimkakati na Kielelezo*

##### *i. Mradi Unganishi wa Liganga na Mchuchuma*

***61.Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2025/2026, Wizara imekamilisha majadiliano na Mwekezaji wa Kampuni *ya Shudao Investment Group Company Limited (SDIG)* kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Chuma cha Liganga na Makaa ya Mawe ya Mchuchuma. Mwekezaji huyu mpya ni Kampuni inayomilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ambayo imeinunua Kampuni awali ya *Sichuan Hongda Group Company Limited (SHG)* kwa lengo la kutekeleza Mradi Unganishi wa Mchuchuma na Liganga kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC).

***62.Mheshimiwa Spika;*** kupitia majadiliano hayo, pande

zote mbili zimefikia makubaliano ya misingi sahihi ya mgawanyo wa hisa na muundo wa uwekezaji (share holders' structure and financing structure); kiwango cha mtaji wa uwekezaji unaohitajika; muundo shirikishi wa usimamizi na uendeshaji wa mradi; muda wa mikataba ya uwekezaji; uhuishaji wa taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi; uandaaji wa modeli ya kifedha ya pamoja; vivutio vya uwekezaji vinavyoendana na sheria za Tanzania; na uongezaji wa thamani kwa madini yote yakiwemo chuma, vanadium, na tatinium hapa nchini. Vilevile, uandaaji wa rasimu za mikataba ya ubia (JVAs) na mikataba ya wanahisa (SHAs) kwa miradi ya uchimbaji na kiwanda cha kutengeneza bidhaa za chuma umekamilika. Kwa ujumla, majadiliano hayo yamekamilika kwa mafanikio makubwa na kwa sasa pande zote zinawasiliana na Mamlaka zao kwa ajili ya hatua za idhini. Hii ni hatua ya kihistoria kwa mradi huu wa kielelezo kwa Taifa letu ambao utakuwa na manufaa makubwa. Aidha, mikataba ya ubia na wanahisa inatarajiwa kusainiwa katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2026/2027 ambapo ujenzi wa miradi unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu.

***63.Mheshimiwa Spika;*** kutekelezwa kwa mradi huo kutawezesha nchi kuokoa matumizi ya dola za Marekani bilioni 1.22 sawa na shilingi trilioni 3.2 ambazo zimekuwa zikitumika kununua bidhaa za chuma kutoka nje ya nchi ikiwa ni bidhaa ya pili kwa matumizi makubwa ya fedha za kigeni baada ya bidhaa za mafuta ya petroli. Vilevile, utekelezaji wa mradi utaongeza mnyororo wa thamani kwa bidhaa mbalimbali zitakazozalishwa kupitia viwanda vingine vitakavyoanzishwa; na utaondoa au kupunguza uharibifu wa miundombinu unaosababishwa na mahitaji ya chuma chakavu katika uzalishaji wa bidhaa za chuma.

***64.Mheshimiwa Spika;*** kwa mujibu wa taarifa za awali za moduli (joint financial model) iliyoandaliwa kwa pamoja na wataalam wa Serikali na mwekezaji, makadirio ya mapato ya Serikali kutokana na kodi mbalimbali pamoja na malipo ya mrahaba kwa kipindi cha miaka 25 ni jumla ya Dola za Marekani trilioni 1.99. Aidha, mapato ya mradi yatatokana na mauzo ya umeme, makaa ya mawe, bidhaa za chuma, titanium, vanadium na aluminium sulphate. Vilevile, utekelezaji wa mradi huu utawezesha kupatikana kwa ajira za moja kwa moja 6,500 na zisizo za moja kwa moja 26,000.

***ii. Mradi wa Magadi Soda Engaruka***

***65.Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia NDC imeendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa kimkakati na kielelezo wa Magadi Soda uliopo katika bonde la Engaruka Wilaya ya Monduli kwa kulipia leseni ya uchimbaji, kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha mradi, na kutafuta mwekezaji. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla shilingi bilioni 5.82 sawa na asilimia 98.7 ya fedha ya fidia ililipwa kwa wafidiwa 513 kati ya wafidiwa 594. Zoezi la kukamilisha ulipaji fidia linaendelea kwa wafidiwa 81 waliobaki ambao wanakamilisha nyaraka zao zikiwemo nyaraka za mirathi. Vilevile, Wizara imefanikiwa kupata mwekezaji na kwa sasa, Timu ya Serikali ya Majadiliano (GNT) inaendelea na majadiliano ya mkataba wa ubia na kampuni iliyoshinda zabuni. Kutekelezwa kwa mradi huo kutaokoa fedha za kigeni zaidi ya dola za Marekani milioni 121 zinazotumika kwa mwaka kuagiza malighafi ya magadi soda pamoja na bidhaa zinazotokana na magadi soda kutoka nje ya nchi.

***iii. Mradi wa Chuma cha Maganga Matitu***

***66.Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia NDC imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maganga Matitu unaotekelezwa kwa

ubia kati ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Kampuni ya Fujian Hexingwang Industry Tanzania Co. Ltd. Hadi kufikia Aprili, 2026 malipo ya fidia yamefanyika ambapo wananchi 380 kati ya 385 sawa na asilimia 98.7 ya wananchi waliopisha mradi, wamelipwa fidia kiasi cha Shilingi bilioni 4.196. Malipo ya fidia kwa wanufaika waliobaki yatafanyika pindi watakapokamilisha taratibu za uhakiki. Kwa sasa, shughuli za kutekeleza mradi zinaendelea ambapo mitambo ya kiwanda imeanza kuingia nchini.

### *B. Kuendeleza miundombinu ya msingi katika Kongani ya Viwanda –TAMCO*

***67.Mheshimiwa Spika;*** Kongani ya Viwanda ya TAMCO iliyopo Kibaha, Mkoa wa Pwani ni kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uzalishaji ikiwemo uunganishaji wa mitambo na magari, uzalishaji wa dawa na vifaa tiba, uzalishaji wa bidhaa nyingine pamoja na huduma saidizi. Eneo hilo lina jumla ya viwanda 14 ambapo viwanda 12 vinafanya kazi na viwili (2) vipo katika hatua ya uwekezaji. Hadi kufikia Aprili, 2026, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu muhimu ikiwemo barabara za ndani kwa kiwango cha lami ambapo kiasi cha kilomita 1.8 zimejengwa. Vilevile miundombinu ya umeme imeboreshwa na wawekezaji wanapata umeme wa uhakika. Viwanda vilivyopo katika Kongani ya TAMCO ni Tanzania Biotech Products Ltd (TBPL) ambayo ni kampuni tanzu ya NDC; Hester Bioscience Ltd; Global Packaging (T) Ltd; Motor Hub East Africa Ltd (TATA Holdings); China Boda Ltd; New Force Company Ltd; Konfa Enterprises; Loti Energies; Hero Sound Traders Ltd; UC General Investment Limited; GF Assemblers Ltd; na Fortes Energies Ltd. Viwanda hivyo kwa pamoja vimetoa jumla ya ajira 853.

**68.Mheshimiwa Spika**; juhudi za Serikali zimeendelea kuvutia wawekezaji zaidi, akiwemo Hyundai Automobile Manufacturing ambaye ameanza maandalizi ya kuanzisha kiwanda cha kuunganisha magari; Goodlife Investment Tanzania anayetarajiwa kuanza uunganishaji wa magari ya umeme (Electric Vehicles); pamoja na Sanda Max Group Limited anayejenga kiwanda cha kuzalisha chakula cha mifugo. Maboresho hayo ya miundombinu yatachochea ukuaji wa uchumi kwa kuongeza fursa za ajira, kukuza mauzo ya nje na kuboresha upatikanaji wa bidhaa kwa gharama nafuu ndani ya nchi.

### C. Kuendeleza kiwanda cha Tanzania Biotec Company Limited (TBPL)

**69.Mheshimiwa Spika**; Tanzania Biotech Products Limited (TBPL) ni kiwanda cha kuzalisha bidhaa za kibaolojia kilichopo Kibaha mkoani Pwani, kinachotumia teknolojia kutoka nchini Cuba kuzalisha bidhaa mbalimbali za kibaiolojia zinazotumika kwenye sekta ya afya, kilimo na mazingira. Kiwanda hiki kinamilikiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 na kina uwezo wa kuzalisha hadi lita milioni sita (6) kwa mwaka. Lengo kuu la uanzishwaji wa kiwanda cha TBPL ni kuzalisha Viuadudu kwa ajili ya kutokomeza ugonjwa wa malaria Nchini Tanzania na barani Afrika ifikapo 2030.

**70.Mheshimiwa Spika**; Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kuimarisha mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria nchini ambapo katika mwaka 2025/2026 jumla ya shilingi bilioni 10.5 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa viuadudu lita 875,000 katika kiwanda cha TBPL. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya lita 491,361 za Viuadudu zimezalishwa ambapo kati ya lita hizo, lita 124,121 zimechukuliwa na Halmashauri 80 nchini. Aidha, uzalishaji na usambazaji wa

viuadudu katika Halmashauri zilizosalia unaendelea. Pamoja na uzalishaji na usambazaji wa viuadudu ndani ya nchi, kiwanda kimeweza kuuza dawa za viuadudu nchi za jirani ikiwemo Uganda zenye thamani ya shilingi milioni 344.07. Hali hii inaashiria kuongezeka kwa imani ya watumiaji na kupanuka kwa soko la dawa hii nje ya Nchi.

***71.Mheshimiwa Spika***; katika kuhamasisha matumizi ya bidhaa rafiki kwa mazingira zisizo na kemikali hatarishi, kiwanda kinaendelea na uzalishaji wa mbolea-hai pamoja na viuatilifu hai ambavyo hutumika kuua wadudu waharibifu wa mazao. Uhaulishaji wa teknolojia za mbolea-hai umekamilika ambapo kiwanda kimezalisha jumla ya lita 3,475 za aina mbili za mbolea hai (Fosforina - lita 1,464 na Dimargon - lita 2011) ambazo kwa sasa zipo katika hatua za majaribio kwenye mazao ya mahindi, matango, nyanya na mbogamboga na zimeonesha ufanisi mzuri. Hadi kufikia Aprili 2026, kiwanda kimefanikiwa kuuza zaidi ya lita 12,000 za viuatilifu hai vinavyotumika kudhibiti wadudu waharibifu kwenye mazao mbalimbali.

### *D. Kuendeleza Kiwanda cha Kilimanjaro Mashine Tools (KMTC)*

***72.Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia NDC imeendelea na juhudi za kukiendeleza na kukisimamia kiwanda cha KMTC Manufacturing Limited kilichopo Kilimanjaro. Hadi kufikia Aprili 2026, kiwanda kimefanikiwa kuzalisha jumla ya mashine 14 na vipuri 159 na kutoa ajira za moja kwa moja kwa vijana 36 na zisizo za moja kwa moja 144. Aidha, jumla ya shilingi milioni 505.69 zimepatikana kutokana na mauzo ya mashine na vipuri hivyo. Kiwanda kwa kushirikiana na Bodi ya Mkonge Tanzania kimefanikisha kubuni na kutengeneza mtambo wa kuchakata katani wenye uwezo wa kuchakata *meta* 80 kwa

siku na kuajiri vijana 10. Katika jitihada za kuongeza uzalishaji wa kiwanda, NDC imefanikiwa kutangaza zabuni ya ununuzi wa mashine ya Steel Grinding Ball Skew Rolling Machine kwa ajili ya kutengeneza golori za kusaga mawe zinazotumika katika vinu katika migodi mikubwa.

### E. Kufanya Tathmini ya Viwanda na Kuainisha Fursa za Uwekezaji

**73. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TIRDO imeendelea kutekeleza zoezi la tathmini ya viwanda na uainishaji wa fursa za uwekezaji wa viwanda nchini. Tathmini hiyo inaainisha idadi ya viwanda, ajira, uwezo wa uzalishaji, teknolojia zinazotumika nchini na maeneo yenye fursa za uwekezaji ili kuchochea maendeleo ya viwanda na kuziongezea thamani rasilimali za ndani. Zoezi hilo limefanyika katika mikoa miwili (2) na hivyo kuwa na jumla ya mikoa tisa (9). Mikoa hiyo ni Pwani, Morogoro, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Manyara, Mwanza na Shinyanga. Aidha, taarifa za viwanda zilizokusanywa kwa mikoa tisa (9) zimeingizwa katika mfumo wa kanzidata za viwanda. Hadi kufikia Aprili, 2026 kanzidata hiyo ina jumla ya viwanda 25,650 ambapo 482 ni viwanda vikubwa, 625 vya kati, 8,980 vidogo na 15,563 ni viwanda vidogo sana.

### F. Kuanzisha na Kuimarisha Maabara kwa Ajili ya Utoaji Huduma

**74. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TIRDO imeendelea kuimarisha na kuboresha maabara kwa ajili ya utoaji huduma za kitafiti katika maendeleo ya viwanda. Katika mwaka 2025/2026 maabara ya chakula ambayo ilipata ithibati mwaka 2025 iliboreshwa kwa kuongeza wigo wa huduma kutoka huduma tatu (3) hadi sita (6) na wigo wa bidhaa kutoka moja

(1) hadi nne (4). Huduma na bidhaa hizo ni pamoja na vyakula vilivyotayari kwa matumizi; nyama na bidhaa zake; samaki na bidhaa zake; na sampuli za usufi wa nyuso (surface swabs). Kuongezeka kwa wigo huo kunaimarisha uwezo wa maabara kutoa huduma jumuishi na za kuaminika zaidi na kupunguza utegemezi wa huduma kutoka nje.

***75.Mheshimiwa Spika;*** vilevile, TIRDO inaendelea na jitihada za kuanzisha Maabara ya Nishati na Madini katika Mkoa wa Njombe ili kusogeza huduma karibu na maeneo yenye rasilimali na shughuli za uzalishaji. Uamuzi huu unatokana na uwepo wa makaa ya mawe katika maeneo ya jirani kama Ludewa, Mbinga na Nyasa na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za upimaji na uthibitishaji wa ubora wa nishati. Maabara hii itahudumia Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Ruvuma, Mbeya na Rukwa) na hivyo kupunguza gharama na muda wa upatikanaji wa huduma. Kupitia maabara hii, vipimo vya ubora wa makaa ya mawe vitahusisha salfa, majivu, maada fukivu, unyevu na thamani ya joto, pamoja na uchambuzi wa elementi na utambuzi wa madini na kemikali, huku pia ikitoa huduma za upimaji wa nishati mbadala ikiwamo mkaa mbadala na biomasi ili kuhakikisha ubora na uendelevu wake.

***76.Mheshimiwa Spika;*** maabara hiyo inatarajiwa kuwa na vifaa vyenye teknolojia ya kisasa itakayowezesha kutoa huduma stahiki kwa jamii. Hadi kufikia Aprili, 2026, Shirika limefanikiwa kumpata mzabuni wa kusambaza na kusimika vifaa hivyo pamoja na kutoa mafunzo kwa wataalam watakaoendesha mitambo hiyo. Kukamilika kwa maabara hiyo kutachochea ongezeko la thamani ya rasilimali za nishati, kuimarisha ushindani wa bidhaa za ndani na kuchochea uchumi wa viwanda unaozingatia nishati safi na rafiki kwa mazingira.

**77.Mheshimiwa Spika;** sambamba na hilo, TIRDO imeendelea na mchakato wa kupata Ithibati kwa maabara za TIRDO. Maabara hizo ni Mazingira, kemia, makaa ya mawe, mafuta na gesi. Katika mwaka 2025/2026, Wizara ilitenga kiasi cha shilingi milioni 100 kwa ajili ya kupata idhibati ya Maabara ya Mazingira. Hatua iliyofikia katika utekelezaji wa mradi huo ni ukamilishwaji wa  mchakato wa manunuzi ya vifaa ambapo mzabuni amepatikana, uandaaji wa nyaraka za ithibati (*quality manual*) pamoja na utoaji wa mafunzo kwa watumishi wa maabara hiyo. Aidha, mchakato wa kupata ithibati kwa maabara za kemia, makaa ya mawe, mafuta na gesi upo katika hatua za awali.

### *G. Uvumbuzi, Utafiti na Uendelezaji Teknolojia*

**78.Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia SIDO imefanikiwa kuhawilisha teknolojia nane (8) za kuchakata mazao mbalimbali. Teknolojia hizo ni utengezaji wa kinu cha kuchoma masalia ya kilimo; mashine ya kutengeneza mkaa mbadala; mashine ndogo ya kusafisha mafuta ya alizeti; mashine za kuzalisha chakula cha samaki; mashine za kusaga mawe yenye madini; mashine za kukamua na kuchuja mafuta ya nazi; mashine za kubangua korosho; na utengenezaji wa *cage* za ufugaji wa samaki kwenye maziwa, mito na bahari.

**79.Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia SIDO imetengeneza mashine tatu (3) za kuzalisha mkaa mbadala kwa kushirikiana na UNIDO ikiwa ni pamoja na kuleta teknolojia mpya kutoka Japani ambazo ni kiwanda cha kuzalisha kuni bora *(briquttes)* katika maeneo ya Ifakara, Morogoro; Kahama, Shinyanga; na Mwanjelwa, Mbeya. Aidha, Mitambo ya kuchuja madini na mchanga na kifaa cha kutoa mchanga katika madini ndani ya mashimo vimetengenezwa katika mikoa ya Lindi, Mbeya na Shinyanga.

**80.Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TEMDO inaendelea kusanifu na kuunda vifaa tiba kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya hospitali. Hadi kufikia Aprili, 2026, TEMDO imefanikiwa kusanifu na kutengeneza vifaa tiba vya aina 15 vilivyoko daraja A ambavyo vimepata ithibati toka Mamlaka ya Uthibiti wa Madawa na Vifaa Tiba (TMDA). Vifaa hivyo ni *bedside locker with stainless steel top (wheeled); bedside locker wooden with stainless steel top (wheeled); bedside locker wooden with wooden top and no wheels; bedside locker wooden with wooden top (wheeled); delivery bed; drip stand with bendbase; drip stand with straight base; examination bed with racks for reclining mechanism; hospital working table (mobile operating table); normal hospital bed (adjusted by slotted bar a ratchet like mechanism); normal hospital bed (adjusted by screw mechanism); normal heavy fixed table; hospital folding screen; na theatre trolleys.* Aidha, kufuatia usanifu huo, vifaa tiba mbalimbali vimetengenezwa vikiwemo vitanda sita (6) vya kujifungulia na vitatu (3) vya kawaida; mitambo 13 ya kuchomea taka ngumu za hospitali; na hifadhi kuta 15 (hospital screen).

**81.Mheshimiwa Spika;** katika jitihada za kutunza mazingira na kuendeleza nishati mbadala, mwaka 2025/2026 TEMDO ilibuni na kutengeneza mashine ya kukausha vumbi la mbao. Mashine hiyo iliyofungwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale katika Mkoa wa Geita ina uwezo wa kuzalisha tani moja (1) ya kuni mbadala kwa siku. Aidha, TEMDO imekamilisha uundaji wa mtambo wa kutengeneza mkaa na kuni mbadala zinazozalishwa kwa kutumia mabaki ya pumba za mpunga ambao umekabidhiwa kwa Halmashauri hiyo. Vilevile, mtambo wenye uwezo wa kuzalisha tani mbili (2) za mkaa mbadala umesanifiwa ambao kwa sasa upo katika hatua ya utengenezaji wa vipuri. Pia, mtambo mwingine wa kutengeneza mkaa na kuni mbadala umesanifiwa na

kutengenezwa na uko tayari kwa ajili ya kuzalisha mkaa mbadala tani moja na nusu (1.5) kwa siku.

***82.Mheshimiwa Spika;*** Wizara, kupitia CAMARTEC, imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za uendelezaji wa teknolojia za kuchakata mazao ya kilimo, mifugo na uchumi wa buluu; na nishati safi ya kupikia. Hadi kufikia Aprili, 2026 CAMARTEC imekamilisha ujenzi wa mitambo miwili (2) ya bayogesi ya ngazi ya taasisi katika kambi za JKT Oljoro na JKT Mafinga. Aidha, CAMARTEC imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa mitambo ya bayogesi katika magereza nane (8) kama awamu ya kwanza kati ya magereza 14 yaliyopangwa kutekelezwa. Magereza hayo ni Mbigiri (Morogoro), Mtego wa Simba (Morogoro), Kingurungundwa (Lindi), Msalato (Dodoma), Ubena (Pwani), Kitai (Ruvuma), Arusha (Arusha), na Bariadi (Simiyu). Lengo la miradi hii ni kutoa nishati safi na endelevu ya kupikia, kupunguza utegemezi wa kuni na mkaa, kulinda mazingira, pamoja na kuboresha usafi na usimamizi wa taka katika maeneo husika.

***83.Mheshimiwa Spika;*** CAMARTEC inaendelea kufanya tafiti katika teknolojia za makaushio ya mboga, matunda na mazao ya uchumi wa buluu; mashine ya kukamua mafuta ya parachichi kwa mkono; mashine za kubangua korosho kwa mkono; mashine ya kutengeneza siagi ya karanga; mashine ya kusaga magunzi na mabua kwa ajili ya mifugo; pamoja na mashine za kuangua mayai. Kukamilika kwa tafiti hizi kutasaidia kuongeza thamani mazao ya kilimo, mifugo na uchumi wa buluu.

***84.Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TIRDO imeendelea kufanya tafiti na kutoa huduma za kitaalamu kwa viwanda kwa kubuni na kuendeleza teknolojia za kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora. Tafiti zilizofanyika zilijikita katika uongezaji

thamani wa malighafi za ndani, ubunifu wa mitambo midogo na ya kati, pamoja na kuboresha ubora wa bidhaa ili kukidhi viwango vya masoko ya ndani na nje. Hadi kufikia Aprili, 2026 Shirika limeunda mtambo wa bayogesi na mtambo wa mkaa mbadala (ECO-Carbonizer) kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya nishati safi.

**85.*Mheshimiwa Spika;*** Utafiti unaohusu ulinzi wa mlaji katika biashara mtandao unaolenga kuchambua hali ya sasa ya ulinzi wa watumiaji katika masoko ya kidijitali. Matokeo ya awali ya utafiti huo yanaonesha uwepo wa pengo katika mfumo wa kisheria, hususan katika kushughulikia changamoto za soko la kidijitali (digital market). Kutokana na hali hiyo, mapendekezo ya maboresho ya sheria yanaandaliwa na yatawasilishwa kwa mamlaka husika, ikiwamo BRELA, BOT na TCRA, kwa ajili ya hatua zaidi. Aidha tafiti zote zilizobaki zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji.

### *3.2.2 Uendelezaji wa Jasiriamali Ndogo na za Kati*

### *A. Kuanzisha na Kuendeleza Viwanda Darasa*

**86.*Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia SIDO imeendelea na juhudi za ujenzi wa viwanda darasa kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati. Katika mwaka 2025/2026 SIDO kwa kushirikiana na KOICA imekalimisha ujenzi wa majengo mawili (2) ya mafunzo ya usindikaji wa vyakula na mahali pa kufanyia uzalishaji katika mikoa ya Dar es Salaam na Morogoro. Hatua inayofuata ni ununuzi wa vifaa na mashine ili majengo hayo yaanze kutumika kwa kazi iliyokusudiwa. Majengo hayo yana uwezo wa kuhudumia wajasiriamali 60 kwa wakati mmoja.

### B. Kuhamasisha na Kuendeleza Uanzishwaji wa Kongani Nchini

**87.*Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wajasiriamali wanaojihusisha na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo katika kongani za *Mbeya Rice Group*, Mkoa wa Mbeya; *Singida Municipal Sunflower Oil Processors Association (SIMSOPA)*, Singida; Magugu-Manyara; na Bitale katika Mkoa wa Kigoma. Hadi kufikia Aprili, 2026 wajasiriamali 95 wamepata mafunzo kuhusu usimamizi wa biashara, uzingatiaji viwango katika uzalishaji na utafutaji wa fursa za masoko ya bidhaa. Aidha, Wizara kupitia SIDO imeendelea kujenga uwezo kwa kutoa mafunzo, ushauri wa kitaalamu, mikopo na mbinu za utafutaji wa masoko kwa wajasiriamali katika kongani 20 kwenye Mikoa ya Geita, Mwanza, Mbeya, Morogoro, Shinyanga, Mtwara na Kagera. Vilevile, Wizara kupitia SIDO imewezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo vipya 296 katika mikoa yote Tanzania na kuchangia jumla ya ajira 1,409.

### C. Kutoa Huduma za Kifedha kwa Wajasiriamali

**88.*Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali (NEDF) unaosimamiwa na SIDO imetoa jumla ya mikopo 829 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.95. Mikopo hiyo imezalisha ajira 1,859 ambapo wanawake ni 957 sawa na asilimia 51 na wanaume ni 902 sawa na asilimia 49 (**Jedwali Na. 15**). Aidha, tangu mfuko ulipoanza kutoa huduma ya mikopo mwaka 1994, hali ya marejesho ya mikopo imekuwa ni ya kuridhisha ambapo wastani wa marejesho ni asilimia 91.1 (**Jedwali Na. 16**). Vilevile, kupitia Programu ya Uwezeshaji Viwanda Vidogo (SANVN Viwanda Scheme), Wizara imewezesha jumla ya wajasiriamali 11 kuunganishwa na Benki ya Azania na kupata mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.98. Halikadhalika,

kupitia Mfuko wa Dhamana ya Serikali (CGS), jumla ya mikopo 18 yenye thamani ya shilingi milioni 422 ilitolewa na Benki ya CRDB.

***89.Mheshimiwa Spika;*** Vilevile, Wizara imepokea kiasi cha shilingi bilioni nne (4) ikiwa ni sehemu ya shilingi bilioni 200 ambazo ni fedha maalum kwa vijana zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya uwezeshaji wa vijana kiuchumi kupitia mikopo. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya maombi 154 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.61 yamepokelewa na taratibu za uchambuzi na uhakiki wa utoaji mikopo hiyo kwa kushirikiana na *CRDB Bank Foundation* unaendelea.

**D. *Utengaji wa Maeneo kwa Ajili ya Shughuli za Wajasiriamali Wadogo na wa Kati***

***90.Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea na juhudi za kuhamasisha utengaji wa maeneo kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati katika mikoa yote nchini. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya hekta 624,584 zimetengwa kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Njombe, Pwani, Rukwa, Shinyanga, Simiyu, Singida, Songwe na Tanga **(Jedwali Na. 17).**

### *3.2.3Mtangamano wa Biashara*

***91.Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kuratibu majadiliano ya kibiashara kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kama ifuatavyo:

## ***A. Nchi na nchi***

### **i. *Utekelezaji wa Mkataba wa Mfumo uliorahisishwa wa ufanyaji Biashara kwa ajili ya kusaidia wafanyabiashara wadogo na wa kati kufanya Biashara za Mpakani kati ya Tanzania, Zambia na Malawi (Simplified Trade Regime-STR)***

***92.Mheshimiwa Spika;*** katika Juhudi za kukuza na kuimarisha biashara ya uwili Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara imeratibu majadiliano na hafla ya utiaji saini wa Mkataba wa Mfumo uliorasimishwa kwa wafanyabiashara wadogo (Simplified Trade Regime – STR) kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Malawi iliyofanyika mwezi Februari, 2026 Jijini Lilongwe – Malawi. Mfumo huo unajumuisha utaratibu maalumu wa biashara unaolenga kurahisisha taratibu za forodha na kupunguza vikwazo visivyo vya kikodi - NTBs kwa bidhaa 61.

***93.Mheshimiwa Spika;*** hatua hii itaimarisha na kurahisisha biashara kwa wafanyabiashara wadogo kupitisha mpakani bidhaa zisizozidi thamani ya dola za Marekani 2,000 kwa siku. Mkataba huo umewezesha wafanyabiashara wadogo kufanya biashara zao kwa urahisi na kupelekea biashara baina ya Tanzania na Malawi kuimarika. Ili kuwa na ufanisi wa utekelezaji wa mkataba huo, Wizara kwa kushirikiana na Chemba ya Taifa ya wafanyabiashara (TNCC) imeendela kutoa Elimu kwa wafanyabishara wadogo wa mpakani. Aidha, mwongozo uitwao ***Kasumulo Business Model*** umeandaliwa ili kutoa utaratibu wa ununuzi na uuzaji wa mazao ya soya, ufuta na mbaazi baina ya Malawi na Tanzania.

**94. *Mheshimiwa Spika;*** kwa upande wa Tanzania na Zambia, nchi hizo zilifanya mkutano wa pili mwezi Desemba 2025 ambapo kupitia mkutano huo, nchi zilikubaliana kuongeza idadi ya bidhaa kutoka 22 hadi 48 zitakazotumika kwenye STR pamoja na nyaraka za forodha (simplified customs document) zitakazotumiwa na wafanyabiashara wanapovuka mpaka wa Tunduma/Nakonde. Kwasasa Serikali inakamilisha taratibu za kusaini Mkataba wa Nyongeza. Utekelezaji wa Mkataba huo unatarajiwa kuongeza mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Zambia na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi kwa wafanyabiashara wadogo ambao wengi ni wanawake na vijana.

**ii. *Mkataba wa Ushirikiano wa Ubia wa Uchumi kati ya Tanzania na Oman***

**95. *Mheshimiwa Spika;*** katika kuimarisha uhusiano wa biashara na kuibua fursa za uwekezaji kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Oman, Wizara iliratibu wadau muhimu walioshiriki katika ziara ya biashara nchini Oman mwezi Aprili, 2025. Ziara hiyo ilifungua fursa za ushirikiano zaidi za uwekezaji katika sekta mbalimbali zikiwemo mifugo, kilimo, usafirishaji na maji. Mafanikio yaliyopatikana katika ziara hiyo ni Taasisi za Sekta Binafsi za nchi zote mbili kukubaliana kuongeza ushirikiano na kuhakikisha fursa za biashara na uwekezaji baina ya Tanzania na Oman zinatumika kikamilifu; kubadilishana uzoefu na teknolojia katika sekta za viwanda na biashara; na kuanzisha majadiliano ya kuingia katika Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi (Comprehensive Economic Partnership Agreement - CEPA).

***96.Mheshimiwa Spika;*** katika hatua ya utekelezaji, Serikali ya Oman imewasilisha Rasimu ya Hadidu za Rejea zenye nia ya kuingia makubaliano ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi (CEPA) na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara imeshafanya uchambuzi wa kina na kuainisha maeneo ambayo Tanzania itakuwa na maslahi nayo na yale ambayo hayastahili kujumuishwa katika Mkataba unaopendekezwa na kuishauri Serikali ipasavyo. Hadidu hizo za rejea zenye maoni ziliwasilishwa Serikali ya Oman mwezi Novemba 2025. Kuridhiwa kwa maoni hayo kutawezesha hatua inayofuata ya majadiliano kuanza.

### iii. *Utatuzi wa Changamoto ya Foleni ya Malori katika Mpaka wa Tunduma, Mkoa wa Songwe*

***97.Mheshimiwa Spika;*** Wizara ilishiriki kikao cha kujadili utatuzi wa changamoto ya foleni ya Malori katika mpaka wa Tunduma, Mkoa wa Songwe, kilichofanyika mwezi Januari 2026, Jijini Dar es Salaam. Kikao hicho kilijadili changamoto za kibiashara katika mpaka wa Tunduma na kukubaliana mpango mkakati wa kutatua changamoto hizo. Mikakati hiyo ni pamoja na mashirika ya Serikali ambayo yana uwezo mkubwa wa kifedha kuingia ubia na sekta binafsi wa kujenga barabara za kulipia (road tolls) kwa utaratibu wa Sheria ya Ubia wa Umma na Sekta Binafsi; TANROADS kukamilisha ujenzi wa kipande cha barabara ya mzunguko katika mpaka wa Tunduma; kuunganisha mifumo ya forodha baina ya Tanzania na Zambia; kuendelea kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari kavu; na kuharakisha upimaji wa mizigo kwa upande wa Zambia kwa kukamilisha ujenzi wa mdaki (scanner) wenye kasi.

**98.Mheshimiwa Spika;** mikakati hiyo imeanza kutekelezwa ambapo kazi ya ujenzi wa kipande cha barabara cha kuingia mpakani kwa njia nne chenye urefu wa mita 750 unaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2026; usimikwaji wa mdaki (scanner) kwa upande wa Zambia umekamilika na tayari umeaanza kufanya kazi, ambapo mdaki huo una uwezo wa kupima lori moja kwa sekunde 30, tofauti na mdaki wa awali ambao ulikuwa unachukua muda mrefu zaidi; uunganishwaji wa mifumo ya TEHAMA baina ya TRA na ZRA unaendelea kwa sasa upo katika hatua ya majaribio; na uendelezaji wa bandari kavu Tunduma kwa sasa timu ya wataalam wa kampuni ya mwekezaji (Jiayou International Logistics) ipo eneo la mradi kufanya upembuzi yakinifu ambapo hatua iliyofikiwa ni asilimia 85. Utekelezaji wa mikakati hiyo utarahisisha biashara baina ya Tanzania, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

### iv. *Uondoaji wa Vikwazo vya Biashara visivyo vya Kiushuru (NTBs)*

**99.Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea kuratibu majadiliano ya masuala ya biashara na uondoaji wa Vikwazo vya Biashara Visivyo vya Kiushuru (Non-Tariff Barriers-NTBs) baina ya Tanzania na nchi za Kenya na Zambia kama ifuatavyo:-

#### *a) Tanzania na Kenya*

**100. Mheshimiwa Spika;** Wizara imefanikiwa kuendelea kutatua vikwazo vya biashara kati ya Tanzania na Kenya kupitia mkutano wa Kamati ya Pamoja ya Biashara (JTC) uliofanyika mwezi Septemba hadi Oktoba, 2025 katika Jiji la Dar es Salaam. Katika mkutano huo, jumla ya vikwazo

vya biashara 14 vilijadiliwa ambapo sita (6) vilihusu malalamiko yaliyowasilishwa na Tanzania na vikwazo nane (8) vilihusu malalamiko yaliyowasilishwa na Kenya. Kati ya vikwazo hivyo 14, vikwazo vitatu (3) vilitatuliwa vilivyohusu ushuru wa bidhaa usio wa haki na tozo kubwa za malipo ya stampu kwenye bia za Tanzania zinapouzwa nchini Kenya. Aidha, changamoto za kusafirisha mbegu kutoka Kenya kuja nchini na tofauti ya gharama ya malipo ya matumizi ya barabara zilitatuliwa.

**101.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika ziara ya Mheshimiwa Dkt William Samoei Ruto Rais wa Jamhuri ya Kenya aliyoifanya nchini tarehe 4 - 5 Mei, 2026. Katika ziara hiyo, wakuu wa nchi za Tanzania na Kenya walielekeza kuondolewa kwa vikwazo vyote vya biashara ndani ya siku 30. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara imewasiliana na taasisi zenye changamoto kwa upande wa Tanzania ili kwa pamoja kuweka mikakati ya namna bora ya kushirikiana na nchi ya Kenya katika kuziondoa changamoto hizo.

### *b) Tanzania na Zambia*

**102.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara ilifanya mkutano wa nne wa Kamati ya Pamoja ya Biashara kati ya Tanzania na Zambia mwezi Agosti, 2025 Nakonde, Zambia. Katika mkutano huo, Vikwazo vya Biashara Visivyo vya Kiushuru (NTBs) 10 vilijadiliwa na nchi zote mbili zilikubaliana muda wa kuondoa vikwazo. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2026 masuala ambayo yametekelezwa baina ya pande zote mbili ni pamoja na kusainiwa kwa Mkataba wa Taasisi zinazohusika na masuala ya vipimo kwa nchi zote mbili (Weight and Measures Agency - WMA na Zambia Metrology Agency - ZMA). Mkataba huo ulisainiwa mwezi Desemba, 2025 kwa lengo la kuondoa

changamoto ya utofauti wa vipimo. Aidha, Hati ya Makubaliano ya ushirikiano wa Mamlaka za Mapato (Revenue Authorities) kwa ajili ya uwianishaji wa mifumo ya forodha na kukamilika kwa maboresho ya miundombinu upande wa Zambia (Nakonde) inayohusisha usimikaji wa mdaki (scanner) mpya wa kisasa na ujenzi wa maegesho yanayochukua malori 75 ilisainiwa. Aidha, Mkutano wa tano (5) umepangwa kufanyika mwezi Mei, 2026.

***103. Mheshimiwa Spika;*** utatuzi wa NTBs kwa kipindi cha hivi karibuni umesaidia kupunguza muda wa kuondosha mizigo mipakani kupitia utekelezaji wa Himaya ya Pamoja ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa upande mwingine utatuzi wa changamoto umewezesha kuendelea na soko la bidhaa kama vile mayai, makaa ya mawe zilizokuwa zimewekewa ushuru wa bidhaa nchini Kenya; kuendelea kwa biashara ya bidhaa za kilimo nchini Malawi ambazo ziliwekewa katazo na nchi hiyo; kuongozeka kwa biashara ya mahindi kwenda nchi jirani kutokana na kutatuliwa kwa malalamiko ya sumu kuvu; kuimarika kwa biashara ya mchele kwenda Uganda na Rwanda kutokana na kuondolewa kwa changamoto iliyokuwa inatolewa na nchi husika kuwa mchele wetu kuchanganywa na mchele kutoka nje ya nchi; na kuruhusiwa mazao ya parachichi na viungo kuingia katika soko la nchi ya Afrika Kusini.

**v. *Utekelezaji wa Tamko la Uanzishaji wa Kamati ya Pamoja ya Biashara (JTC) kati ya Tanzania na Uturuki***

***104. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea na jitihada za kuongeza kiasi cha biashara kati ya Tanzania na Uturuki ili kufika dola za Marekani Bilioni 1, kama yalivyokuwa

makubaliano katika kikao cha Wakuu wa Nchi za Tanzania na Uturuki. Makubaliano hayo yalifikiwa wakati wa ziara ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Uturuki mwezi Aprili, 2024. Tarehe 23 Julai 2025 Serikali zote mbili zilisaini Tamko la kuanzisha Kamati ya Pamoja ya Biashara (Joint Trade Committee) kwa ajili ya kujadili fursa za biashara zilizopo baina ya Uturuki na Tanzania na kuweka mikakati ya kutumia fursa hizo na hatua nyingine za utekelezaji.

**B. Kikanda**

***i. Utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA)***

***105. Mheshimiwa Spika;*** katika utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA), Wizara imeendelea kushiriki katika majadiliano ya biashara kupitia Mpango wa Majaribio ya Biashara (Guided Trade Initiative - GTI) ambapo kampuni za Tanzania zimefanikiwa kufikia masoko mapya na kupata uzoefu wa moja kwa moja katika taratibu za forodha. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya kampuni 40 za Tanzania zimefanya biashara kwa kutumia Vyeti vya Uasili wa Bidhaa vya AfCFTA, ambapo jumla ya vyeti 500 vimetolewa. Kupitia soko hilo, mauzo ya Tanzania kwenda Ghana yalikuwa na thamani ya dola za Marekani Milioni 62.9; Nigeria dola za Marekani Milioni 8; Algeria dola za Marekani Milioni 3.7; na mauzo kwenda Misri yalikuwa ya dola za Marekani Milioni 1.1. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni nyuzi za katani ambazo zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 56, ikifuatiwa na kahawa na viungo ambavyo vilikuwa na jumla ya dola za Marekani milioni 3 na vioo (float glasses) ambavyo vilikuwa na dola za Marekani milioni 2.4.

***106. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imekamilisha na kuzindua Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (National AfCFTA Implementation Strategy) mwezi Julai, 2025. Aidha, Timu ya Kitaifa ya kusimamia utekelezaji wa Mkakati huo imeshaundwa ikihusisha wadau wa sekta ya umma na sekta binafsi. Vilevile, Wizara imekamilisha Mwongozo wa Hatua kwa Hatua wa Ufanyaji Biashara chini ya Eneo Huru la Biashara Afrika ambao utasaidia jamii ya wafanyabiashara kujua kwa kina hatua wanazopaswa kuzifuata wakati wa kuagiza na kuuza bidhaa kwenye soko hilo.

### ii. *Mkutano Maalum wa 59 wa Baraza la Mawaziri wa EAC na Mkutano wa 25 wa* Wakuu wa Nchi.

***107. Mheshimiwa Spika;*** Mkutano Maalum wa 59 wa Baraza la Mawaziri wa EAC ulifanyika mwezi Aprili, 2026 jijini Arusha na kufuatiwa na Mkutano wa 25 wa wakuu wa nchi. Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kujadili taarifa ya mwaka ya Baraza la Mawaziri wa EAC; uzinduzi wa Mkakati wa saba wa maendeleo wa EAC; uzinduzi wa dhamana ya forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; na masuala mengine. Mikutano hiyo inachangia katika kuchochea maendeleo ya Sekta ya Viwanda na Biashara nchini, hususan uzinduzi wa Mkakati wa Saba wa Maendeleo wa EAC (2026/27–2030/31) ambao umeweka vipaumbele katika kuimarisha biashara ya kikanda, kuongeza uzalishaji na thamani ya bidhaa na kuboresha ushindani wa bidhaa za viwanda vya ndani na nje ya nchi. Aidha, uzinduzi wa Dhamana ya Forodha ya EAC utarahisisha usafirishaji wa bidhaa ndani ya Jumuiya kwa kutumia dhamana moja hivyo kupunguza gharama za biashara, kuongeza ufanisi wa forodha na kufungua fursa zaidi za masoko kwa wazalishaji na wafanyabiashara wa Tanzania ndani na nje ya nchi.

***108. Mheshimiwa Spika;*** maendeleo katika kuimarisha Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja na tathmini ya Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi (EPA), yanaipa Tanzania nafasi ya kulinda na kukuza viwanda vya ndani huku ikinufaika na masoko ya kikanda na kimataifa. Uteuzi wa mwakilishi wa Tanzania katika Tume ya Ushindani ya EAC utaimarisha usimamizi wa ushindani wa haki katika biashara na hivyo kuboresha mazingira ya uwekezaji. Kwa ujumla, maamuzi ya mikutano hiyo yanaongeza ufanisi wa mifumo ya kikanda na kufungua fursa mpya kwa Serikali katika kuimarisha utekelezaji wa sera na mipango ya kukuza viwanda na biashara nchini.

**C. Kimataifa**

***i. Utekelezaji wa Mkataba wa Uwezeshaji Biashara wa Shirika la Biashara Duniani (WTO Trade Facilitation Agreement – TFA) na Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara (NCTF)***

***109. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara (National Committee on Trade Facilitation (NCTF), inaendelea na utekelezaji wa Mkataba wa Uwezeshaji Biashara wa Shirika la Biashara Duniani ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na wadau wa maendeleo kwa ajili ya ufadhili wa miradi iliyoandaliwa na utekelezaji wa Mkataba kwa ujumla. Aidha, Kamati inaendelea kufanya mapitio ya Mpango Mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Kamati wa miaka mitano (National Trade Facilitation Roadmap Review). Maandalizi ya mpango huo yamefikia katika hatua ya kukusanya maoni kutoka kwa wadau.

**110. Mheshimiwa Spika;** Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara imeendelea kutatua changamoto za wafanyabiashara kupitia kliniki ya wafanyabiashara hasa katika mpaka wa Tunduma. Kupitia kliniki hiyo wafanyabiashara wamepatiwa uelewa kuhusu taratibu za kuvuka Mipakani; kutumia mfumo uliorahisishwa kwa wafanyabiashara wadogo; uondoshaji na upitishaji wa mizigo mipakani na usafirishaji; na taratibu na fursa za biashara ya kikanda. Kupitia mpango huu jumla ya wafanyabiashara 72 wamenufaika na mafunzo hayo.

***ii. Mkutano wa Biashara wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo – UNCTAD***

**111. Mheshimiwa Spika;** Mkutano wa Biashara wa UNCTAD ni mkutano ambao hufanyika kila baada ya miaka minne unaowakutanisha Wakuu wa Nchi, Mawaziri wa Biashara na Uchumi, Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa na Wataalam wa masuala ya Biashara kwa lengo la kujadili biashara na maendeleo katika kuwezesha uchumi imara na endelevu ya nchi wanachama. Mkutano wa 16 ulifanyika mwezi Oktoba, 2025 Geneva, Uswisi. Majadiliano katika mkutano huo yalihusu viwango vya usalama wa bidhaa za watumiaji na mapendekezo yakiwa ni kuimarisha usalama wa bidhaa kupitia mageuzi ya kitaifa na kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa. Vipaumbele muhimu vilivyoafikiwa ni pamoja na kuimarisha mifumo ya udhibiti; kuboresha tathmini ya hatari na ukusanyaji wa taarifa; kuimarisha mifumo ya kubadilishana taarifa za kuvuka mipaka; na kuzingatia mahitaji mahsusi ya nchi zinazoendelea.

### iii. Uratibu na Uwasilishaji wa Taarifa mbalimbali za Biashara katika Shirika la Biashara Duniani (WTO Notifications)

**112. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara huwasilisha taarifa mbalimbali zinazohusu biashara katika Shirika la Biashara Duniani (WTO) kupitia mfumo maalum wa *e-ping.* Taarifa hizo zinahusu masuala ya vigezo vya viwango; afya ya wanyama, mimea na usalama chakula; masuala ya ruzuku katika biashara; na ushuru wa mipakani. Hadi kufikia Aprili, 2026 Tanzania imeendelea kufanya vizuri WTO ambapo jumla ya taarifa (notification) 506 ziliwasilishwa katika shirika hilo kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje ya Nchi. Aidha, katika kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2021 hadi 2025, Tanzania imefanikiwa kuwa miongoni mwa nchi 10 kati ya nchi 166 wanachama wa WTO zinazowasilisha taarifa za biashara katika shirika hilo katika eneo la Vikwazo vya Biashara vya Kiufundi (Technical Barrier to Trade - TBT). Hali hiyo inaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazozingatia misingi ya uwazi katika biashara Duniani.

## 3.2.4 Maendeleo ya Biashara

### A. Kuboresha Mazingira ya Biashara

**113. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea na jukumu la kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini ambapo katika mwaka 2025/2026 Wizara imefanikiwa kudhibiti raia wa kigeni kufanya biashara zinazostahili kufanywa na Watanzania kupitia Tangazo la Serikali Na. 487A la tarehe 28 Julai, 2025. Tangazo hilo linatoa katazo kwa raia wa kigeni kujihusisha na biashara 15 zinazostahili kufanywa na Watanzania. Biashara hizo ni pamoja na uuzaji wa bidhaa kwa jumla na rejareja, huduma za watalii wa ndani, huduma

za fedha kwa njia ya simu (Mawakala), saluni, usafirishaji wa mizigo, uuzaji wa vinyago, uchimbaji mdogo wa madini, uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya redio na runinga, uendeshaji wa viwanda vidogo, kampuni za huduma ya usafi na uuzaji wa nyumba na viwanja.

***114.*** ***Mheshimiwa Spika;*** katika utekelezaji wa Sheria ya Katazo hilo, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali imechukua hatua madhubuti za kisera, kisheria na kiutendaji ambapo hadi kufikia Aprili, 2026, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imezuia uhuishaji wa leseni za biashara 907. Kati ya hizo, leseni 737 ni za biashara za uingizaji na uuzaji wa bidhaa, leseni tano (5) katika huduma za posta na utoaji wa vifurushi ndani ya mipaka ya kitaifa, leseni 119 za uwakala au udalali katika biashara na sekta ya mali isiyohamishika na leseni 46 za huduma ya utoaji na usafirishaji wa shehena. Hatua hii imerejesha imani ya wazawa kwa Serikali kwa namna inavyosaidia kutatua changamoto za kibiashara; imeboresha mazingira ya biashara kwa wazawa na hivyo kuongeza uwekezaji kwenye biashara; na imeongeza uwezo wa ushindaji kwa wazawa kwenye biashara. Katika kuboresha utekelezaji wa katazo hilo, Serikali imefanya marejeo na kuandaa rasimu ya katazo ambayo ipo katika hatua ya uidhinishwaji.

***115.*** ***Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya maombi 373 ya vibali vya kazi kwa raia wa kigeni wanaokuja kufanya kazi nchini katika tasnia ya biashara hayakuidhinishwa kutokana na kutokukidhi vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria. Vilevile, Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam na Mbeya zimezuia uhuishaji wa leseni za biashara 191 kwa biashara ya uuzaji wa bidhaa kwa jumla, uuzaji wa bidhaa kwa rejareja, uchimbaji mdogo wa madini na biashara ya maghala/stoo ambazo zinamilikiwa na

wafanyabiashara/kampuni wasio raia wa Tanzania kwa kuzingatia amri iliyotolewa. Biashara 13 kati ya 191 zilizozuiwa kuhuishwa au kupewa leseni zilikuwa katika eneo la kariakoo.

***116. Mheshimiwa Spika;*** katika jitihada za kuendelea kuimarisha diplomasia ya uchumi, Wizara iliratibu Majadiliano ya Tatu ya Biashara kati ya Tanzania na Japan yaliyofanyika mwezi Novemba, 2025 Jijini Dar es Salaam kwa dhumuni la kuimarisha mahusiano ya biashara na uwekezaji na kutatua changamoto mbalimbali za wafanyabiashara na wawekezaji kutoka Tanzania na Japan. Katika majadiliano hayo, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za serikali ilitoa ufafanuzi wa changamoto tatu (3) zilizowasilishwa na Ofisi ya Ubalozi wa Japan ambazo zilihusu utoaji wa viza, vibali vya kazi na makazi; taratibu za ukusanyaji wa kodi; na masuala ya ushindani wa haki katika soko.

### *B. Kukuza Biashara za Watanzania kupitia Kliniki*

***117. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea na jitihada za kukuza biashara za watanzania kupitia taasisi zake ambapo katika mwaka 2025/2026 Wizara imetoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kurasimisha biashara msisitizo ukiwekwa katika usajili, leseni, pamoja na mabadiliko ya sheria zinazosimamiwa na BRELA. Elimu hiyo imetolewa kupitia njia mbalimbali zikiwemo vyombo vya habari, maonesho na mikutano. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wakala ilitoa mafunzo kwa wadau walioshiriki maonesho sita (6) ya kibiashara. Maonesho hayo ni maonesho ya Wakulima Nanenane; Tiba Asili; Biashara Afrika Mashariki; Madini; Mamlaka ya Usafiri wa Ardhini; na Maonesho ya Tiba Lishe ambapo kupitia maonesho hayo takribani wadau 27,000 walielimishwa.

***118. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia BRELA ilitoa elimu kupitia kliniki za biashara zilizofanyika katika mikoa mbalimbali kwa nyakati tofauti, zikiwemo kliniki ya biashara katika Mkoa wa Mwanza wakati wa michezo ya SHIMIWI, kliniki ya biashara katika Mkoa wa Dar es Salaam wakati wa maonesho ya Wiki ya Huduma kwa Mteja pamoja na kliniki za biashara wakati wa michezo ya SHIMMUTA katika Mkoa wa Morogoro. Kwa upande wa vyombo vya habari, BRELA ilitoa elimu kupitia vipindi nane (8) vya luninga, vipindi 20 vya redio, pamoja na uchapishaji wa taarifa 23 katika magazeti.

***119. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TanTrade imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma za usaidizi kibiashara kupitia kliniki za Biashara ambapo jumla ya wadau 986 walihudumiwa katika majukwaa mbalimbali ya maonesho. Kupitia kliniki hizo jumla ya changamoto 192 ziliwasilishwa ambapo 191 zilipatiwa ufumbuzi kupitia TanTrade na SIDO; kampuni 137 zilisajiliwa na BRELA na BPRA; kampuni 107 zilipata elimu ya uzalishaji bora na alama za ubora kupitia TBS na WMA. Kupitia kliniki hizo, wadau 32 walipata ufahamu wa taratibu za vibali vya kemikali kupitia GCLA; wafanyabiashara 45 waliunganishwa na masoko ya kitaifa na kimataifa; kampuni 41 zilishauriwa kuhusu mashine, vifungashio na mikopo; kampuni 79 zilipata elimu ya kodi na kampuni saba (7) zilipata TIN kupitia TRA; na kampuni tano (5) ziliunganishwa na kampuni ya Islamabad kutoka Pakistani kwa ajili ya kuuza tani 300 za maharage.

### C. Kutayarisha Viwango vya Kitaifa Katika Sekta/Nyanja Mbalimbali

***120. Mheshimiwa Spika*;** Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imekamilisha viwango muhimu pamoja na viwango mbalimbali katika Sekta ya Kilimo,

Chakula na Uhandisi. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya viwango 230 vilitayarishwa. Aidha, jumla ya viwango 499 vipo kwenye hatua za mwisho za maandalizi ambapo vitakamilika ndani ya mwaka 2025/2026.

### *D. Kutoa Leseni ya Ubora Kwa Bidhaa Katika Sekta Mbalimbali Zikiwemo Bidhaa za Wajasiriamali Wadogo*

***121. Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya leseni 856 za nembo ya ubora ya TBS zilitolewa sawa na asilimia 85.6 ya lengo la kutoa leseni 1,000 kwa mwaka. Miongoni mwa leseni hizo, leseni 349 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo wanaozalisha bidhaa mbalimbali kama vile siagi ya karanga, asali, maji ya kunywa, pombe kali (spirit), vifungashio, mchele na pombe nyingine. Shirika limeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali na wadau mbalimbali katika dhana nzima za kuzingatia mifumo ya ubora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora.

### *E. Kusajili Majengo, Maeneo ya Uzalishaji, Uuzaji na Usambazaji wa Bidhaa za Chakula na Vipodozi*

***122. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TBS imeendelea na huduma za kusajili majengo yanayohifadhi bidhaa za chakula na vipodozi kwa lengo la kuhakiki ubora na ufanisi wa maeneo hayo ili kuendelea kulinda afya za walaji. Hadi kufikia Aprili 2026, TBS imesajili majengo, maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi 31,598 sawa na asilimia 87.8 ya lengo la kusajili na kutoa vibali 36,000 kwa mwaka. Kati ya maeneo yaliyosajiliwa, maeneo 27,295 yanajihusisha na chakula na maeneo 4,303 yanajihusisha na vipodozi.

### *F. Kusajili Bidhaa za Chakula na Vipodozi*

***123.*** ***Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia TBS imesajili bidhaa za chakula na vipodozi 2,070 ambavyo ni sawa na asilimia 86.3 ya lengo la kusajili na kutoa vibali 2,400 kwa mwaka. Kati ya bidhaa hizo, bidhaa 1,406 ni za chakula na bidhaa 664 ni za vipodozi.

***124.*** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kuhakikisha bidhaa za chakula na vipodozi zina ubora unaotakiwa, Wizara kupitia TBS imesogeza huduma zake karibu na wananchi kwa kuanzisha ofisi katika kanda tisa (9); ujenzi wa maabara katika kanda ya kati Dodoma na kanda ya ziwa Mwanza. Aidha, Wizara inaendelea na taratibu za kumpata mkandarasi wa kujenga maabara katika kanda ya kaskazini Arusha. Vilevile Wizara imeendelea kusajili bidhaa zinazozalishwa ndani na zile zinazoingia nchini; na kuendelea na utoaji wa ithibati ya bidhaa za chakula na vipodozi kwa kufanya tathmini na kaguzi za awali wa kiwanda na kufanya kaguzi endelevu za bidhaa sokoni.

### G.*Kukagua na Kutoa Vibali kwa Bidhaa Zitokazo Nje ya Nchi*

***125.*** ***Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya vyeti vya ubora 128,430 vimetolewa kwa shehena za bidhaa zinazotoka nje ya nchi ambayo ni sawa na asilimia 91.7 ya matarajio ya kutoa jumla ya vyeti vya ubora wa bidhaa 140,000 kwa mwaka. Kati ya vibali hivyo, vibali 40,225 ni kwa bidhaa zilizokaguliwa nje ya nchi na vibali 88,205 ni kwa bidhaa zilizokaguliwa nchini. Aidha, jumla ya magari 50,919 yaliyotumika nje ya nchi yalikaguliwa sawa na asilimia 101.8 ya lengo la kukagua magari 50,000 kwa mwaka.

### H. Kuthibitisha Kampuni Chini ya Mifumo ya Ubora na Uongozi

**126.** ***Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya kampuni 15 zilithibitishwa kuwa na mifumo yenye ubora wa kimenejimenti sawa na asilimia 93.8 ya lengo la kuthibitisha kampuni 16 kwa mwaka.

### I. Kupima Sampuli za Bidhaa Mbalimbali na Kufanya Ugezi kwa Vifaa/Mashine Mbalimbali

**127.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kusimamia ubora wa bidhaa, Wizara kupitia TBS hupima ubora wa bidhaa kwa kupitia sampuli zinazoletwa kwenye maabara. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya sampuli 40,444 zilipimwa katika maabara mbalimbali za TBS kwa lengo la kuhakiki ubora ambayo ni sawa na asilimia 101.1 ya lengo la kupima sampuli 40,000 kwa mwaka. Aidha, Shirika hupima bidhaa za wazalishaji ili kuhakiki ubora na usalama wa bidhaa hizo kabla ya matumizi.

**128.** ***Mheshimiwa Spika;*** vilevile, Shirika limefanya ugezi (calibration) wa vifaa/mashine mbalimbali ambapo hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya vifaa 12,444 vilifanyiwa ugezi ambavyo ni sawa na asilimia 103.7 ya lengo la kufanya ugezi wa vifaa 12,000 kwa mwaka. Lengo la kufanya ugezi wa mitambo au vifaa mbalimbali vinavyotumika katika uzalishaji wa bidhaa ni kuhakikisha usawa/usahihi wa vipimo wakati wa matumizi ya vifaa hivyo.

### J. Kuweka Kinasaba Katika Kusimamia Ubora wa Bidhaa

**129.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TBS imeendelea kutekeleza jukumu la kuweka kinasaba kwenye

mafuta ambapo hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya lita bilioni 4.35 za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa ziliwekewa kinasaba sawa na asilimia 90.8 ya lengo la kuweka kinasaba katika lita bilioni 4.8 za mafuta kwa kipindi cha mwaka. Lengo la kuweka kinasaba ni kuendelea kudhibiti ubora wa mafuta pamoja na upotevu wa mapato ya Serikali kwa kuuza mafuta yasiyolipiwa kodi katika soko la ndani. Aidha, mafuta ambayo hayawekewi kinasaba ni yale yanayosafirishwa kwenda nchi jirani na mafuta yenye msamaha wa kodi yanayotumika kwenye miradi maalum.

### *K. Kupata Ithibati ya Umahiri ya Kiwango cha Kimataifa cha ISO/IEC 17020*

***130. Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2025/2026, TBS, ilifanikiwa kupata ithibati ya umahiri (accreditation) ya kiwango cha kimataifa cha ISO/IEC 17020 katika ukaguzi wa bidhaa ambayo ilitolewa na taasisi ya Huduma za Umahiri ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika yaani SADCAS. Hatua hiyo imepelekea TBS kuwa taasisi ya kwanza nchini na ya pili kwa ukanda wa Afrika Mashariki kupata ithibati hiyo. Ithibati ya umahiri wa mfumo wa ukaguzi katika kiwango cha kimataifa ni hatua muhimu na ya kimkakati inayoiwezesha nchi yetu kuepuka vikwazo vya kiufundi katika biashara, kuaminika kwa matokeo ya udhibiti na kurahisisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa ndani na nje ya nchi na hivyo kukuza uchumi wa Taifa.

### *L. Udhibiti wa Bidhaa za Bandia*

***131. Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia FCC imefanikiwa kutekeleza operesheni maalum za udhibiti katika bidhaa mbalimbali ikiwemo pombe bandia. Katika operesheni zilizofanyika katika mkoa wa Dar es

Salaam, jumla ya chupa 4,251 za vinywaji bandia pamoja na chupa tupu 286 na katoni tupu 250 zilikamatwa. Aidha, vifaa vya uzalishaji na ufungashaji vilikamatwa, ikiwemo mashine za kuchapisha maelezo ya bidhaa, kipima kilevi, mashine ya kufunga vifuniko, mizani, ethanoli, vyombo vya kuchanganyia na kuchujia pombe. Aidha, FCC imebaini uwepo wa bidhaa nyingine bandia za vipuri na vilainishi ambazo zilikamatwa na watuhumiwa kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria. Mkakati wa Wizara kupitia FCC katika kukabiliana na tatizo la bidhaa bandia unalenga kuimarisha uchunguzi wa taarifa za kiintelijensia, utekelezaji wa operesheni za ukaguzi na ukamataji pamoja na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wahusika.

***132. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) mwaka 2024/2025 ilifanya utafiti na kubaini uwepo wa mwenendo wa unywaji holela wa pombe miongoni mwa jamii unaoweza kusababisha athari za kiafya, kiuchumi na kijamii. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia TBS imeendelea kutoa elimu kwa jamii kwa kushirikiana na Idara zingine za Serikali (Maendeleo ya Jamii, Afya) juu ya athari za matumizi holela ya pombe. Matarajio ni kuhakikisha wananchi wanatumia kwa usahihi bidhaa za pombe zinazokidhi matakwa ya ubora na usalama. Elimu hiyo imetolewa katika mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Dodoma na Mwanza. Hivyo, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wengine katika kudhibiti mienendo hiyo.

### M. Kusajili Kampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma, Hataza na Vyeti vya Usajili wa Viwanda

***133. Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imefanikiwa kusajili jumla ya kampuni 16,864, kati ya 19,640 zilizokusudiwa, sawa na asilimia 86. Majina ya Biashara 30,631 yalisajiliwa kati ya 33,800 yaliyopangwa, ambayo ni sawa na asilimia 91 ya lengo. Katika eneo la Alama za Biashara na Huduma, alama 2,804 zilisajiliwa kati ya 3,600, sawa na asilimia 78 ya lengo la mwaka. Kwa upande wa maombi ya Hataza, Wakala ilitoa Hataza 44 kati ya 40 zilizolengwa, sawa na asilimia 110 ya makadirio. Sambamba na hayo, Wakala ilitoa Vyeti vya Usajili wa Viwanda 42 kati ya 65 vilivyokusudiwa, ambavyo ni asilimia 65 ya utekelezaji.

***134. Mheshimiwa Spika;*** katika kurahisisha mazingira ya kufanya biashara nchini, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wadau wengine imeendelea kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali. Sheria zilizofanyiwa mapitio ni pamoja na Sheria ya Kampuni Sura ya 212, Sheria ya Majina ya Biashara Sura ya 213, Sheria ya Alama za Biashara na Huduma Sura ya 326, Sheria ya Usajili wa Hataza Sura ya 217, na Sheria ya Alama za Bidhaa Sura ya 85. Mapitio ya Sheria hizi zote yamekamilika na zipo katika hatua za uidhinishwaji.

### N. *Kutoa Leseni za Biashara kundi ‘A’ na za Viwanda*

***135. Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia BRELA imefanikiwa kutoa jumla ya Leseni za Viwanda 512 kati ya 437 zilizopangwa, sawa na asilimia 117 ya lengo. Aidha, Leseni za Biashara kundi “A” 19,110

zilitotolewa kati ya 21,582 zilizokusudiwa, ikiwa ni asilimia 89 ya utekelezaji. Mafanikio haya yanadhihirisha jitihada endelevu za Serikali katika kuimarisha na kurahisisha usimamizi na udhibiti wa taratibu za biashara zinazozingatia matakwa ya kisheria. Kutokana na maboresho yaliyofanyika katika mifumo ya usajili wa biashara na leseni, mteja anaweza kukamilisha taratibu za usajili na kupata cheti cha jina la biashara ndani ya siku moja, leseni siku mbili na kampuni siku tatu za kazi.

### *O. Kufanya Kaguzi Elimishi za Leseni Za Biashara Kundi 'A' na Viwanda*

***136. Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia BRELA imefanya kaguzi elimishi tatu (3) kati ya hizo mbili zilifanyika kwenye eneo la Leseni za Biashara kwa wafanyabiashara wa kigeni katika Soko la Kariakoo, Jijini Dar es Salaam. Jumla ya biashara za kigeni 37 zilikaguliwa, kati ya hizo, biashara 36 zilikuwa na leseni halali za biashara na biashara moja (1) ilikuwa na leseni ya biashara iliyokwisha muda wake. Kati ya biashara zilizokaguliwa, biashara 12 zilikuwa na leseni za kundi 'B' na 24 kundi 'A'. Aidha, ukaguzi wa tatu (3) ulifanyika mkoa wa Pwani. Hatua zilizochukuliwa kwa biashara ambazo hazina Leseni ni pamoja na kutoa elimu kwa wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa kufanya biashara kwa kufuata Sheria za Nchi na walipatiwa Leseni.

***137. Mheshimiwa Spika;*** vilevile, kaguzi elimishi kwa Wamiliki Manufaa (Beneficial Ownership) wa kampuni zilifanyika Jijini Dar es Salaam na Arusha ambapo kampuni 632 zilitembelewa. Kati ya kampuni hizo, kampuni 398 sawa na asilimia 63 zilikuwa zimewasilisha taarifa za wamiliki manufaa na kampuni 562 sawa na asilimia 89 zilikuwa zimelipa ada za mwaka (annual return).

### *P. Kuendelea Kuboresha na Kuimarisha Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA kwa Ajili ya Kuboresha Utoaji wa Huduma*

***138. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia BRELA imeendelea kuimarisha ulinzi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa kufanikiwa kukamilisha mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kujikinga na Majanga ya kimtandao. Sambamba na hilo, BRELA imetoa elimu kwa watumishi 119 kuhusu ulinzi wa taarifa mtandaoni na namna ya kuzuia uharibifu katika mfumo unaotokana na majaribio ya udukuzi wa taarifa. Aidha, Wakala imeendelea kufanya maboresho katika mifumo ya Usajili kwa njia ya Mtandao (Online Registratioin System - ORS) na Tanzania National Business Portal – TNBP, Industrial Property Automation System – IPAS na kuifungamanisha na mifumo mingine ya Serikali inayosimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA). Lengo likiwa ni kuleta urahisi wa huduma kufikiwa na wateja na kuondoa kero zinazoathiri kasi ya utekelezaji wa majukumu ya usajili kwa njia ya mtandao.

### *Q. Kutoa Leseni na Kufanya Ukaguzi wa Ghala*

***139. Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), imetoa jumla ya leseni 367 za Waendesha Ghala na leseni mbili (2) za Wakaguzi wa ghala katika msimu wa mwaka 2025/2026. Aidha, Bodi imefanikiwa kukagua jumla ya ghala 734 za kuhifadhia mazao kabla ya msimu kuanza na wakati msimu unaendelea. Vilevile, Bodi imefanikiwa kuratibu uuzwaji wa kilo 953,913,595 za mazao ya korosho, mbaazi, ufuta, dengu, choroko, kakao, na soya yenye thamani ya shilingi trilioni 2.14 **(Jedwali Na.18).**

### *R. Kufanya upanuzi wa Utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa Kuongeza Bidhaa za Kilimo na Zisizo za Kilimo Katika Mfumo*

***140. Mheshimiwa Spika;*** Bodi imeendelea kuongeza wigo wa matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika Sekta mbalimbali za uzalishaji nchini. Hadi kufikia Aprili, 2026 mfumo una bidhaa 15 za kilimo ambazo ni Korosho, Ufuta, Mbaazi, Dengu, Choroko, Mahindi, Mpunga, Mchele, Vitunguu swaumu, Maharage, Chai, Kahawa, Kakao, Karanga na Mhogo mkavu na moja (1) isiyo ya kilimo ambayo ni Asali. Katika kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, Bodi imewezesha kufungwa kwa kamera za CCTV katika ghala 54 katika mikoa ya Lindi, Pwani na Mtwara. Zoezi hili linaendelea kutekelezwa katika maghala yote yanayotumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala nchini.

***141. Mheshimiwa Spika;*** ili kuboresha uwazi na ujumuishi katika utekelezaji wa shughuli za mfumo wa stakabadhi za ghala, Bodi imeendelea kufanya usaili wa waendesha ghala kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Bodi za Mazao, Soko la Bidhaa Tanzania, Tume ya Maendeleo ya Ushirika, vyama vya msingi (AMCOS), Ofisi ya Mkoa na Halmashauri katika utaratibu mzima wa upatikanaji wa Waendesha Ghala Mahiri. Zoezi hili limekuwa hatua muhimu katika kujenga uwazi na kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa mfumo na hata kurahisisha utatuzi wa changamoto pale zinapojitokeza.

***142. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia WRRB imeendeleza jitihada za kuongeza bidhaa mbalimbali nchini katika mfumo wa stakabadhi za ghala na ujumuishi wa sekta binafsi kwa kushughulikia kikwazo cha waweka mali ghalani kukosa mikopo kutoka taasisi za fedha kwa kutumia

stakabadhi za ghala. Ili stakabadhi za ghala zitumike kama dhamana kwenye taasisi za fedha, kunahitaji Mameneja Dhamana wa taasisi za fedha kuwa na weledi wa utoaji wa dhamana katika stakabadhi za ghala. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa tarehe 17 Aprili 2026 Benki Kuu ya Tanzania ilirasimisha utaratibu wa Meneja Dhamana chini ya mfumo wa stakabadhi za ghala kwa kutoa Mwongozo kwa taasisi za fedha kuwa na Mameneja Dhamana wenye leseni kutoka Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala.

***143. Mheshimiwa Spika;*** katika kuongeza ufanisi kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala inaendelea kuunganisha mifumo yake na mifumo ya wadau wengine kama vile Soko la Bidhaa (TMX), Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) na Bodi ya Korosho. Muunganiko huu utaongeza ufanisi katika utendaji kazi na kuwa kichocheo cha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati zitakazotumika katika soko.

***144. Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2025/2026 Bodi imeendelea kuwa kichocheo cha uzalishaji na ufanyaji wa biashara kwa mikoa ambayo haikuwahi kuuza bidhaa ya korosho kupitia mfumo wa stakabadhi za ghala. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Mkoa wa Singida umeuza zao la korosho kupitia mfumo huu katika msimu wa 2024/2025 ambapo uliuza tani 128.7 (kwa mara ya kwanza) na msimu wa 2025/2026 tani 541.12 ikiwa ni ongezeko la asimilia 320.12. Hii inaashiria kuwa mfumo huu unakuwa kichocheo katika kufanya biashara ya bidhaa na kuwakomboa Watanzania walio wengi kwa kuwa zao hili lilizoeleka kuwa ni zao la Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Ruvuma.

***145. Mheshimiwa Spika;*** Bodi imeendelea kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi. Katika

mwaka wa fedha 2025/2026 Bodi imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda kwa kuhamasisha muunganiko baina ya taasisi zinazofanya kazi za usimamizi wa mfumo huu katika ukanda wa Afrika Mashariki. Muunganiko huu ni nyenzo muhimu ya kukuza biashara kati ya Tanzania na nchi jirani, ikizingatiwa kuwa Tanzania ni moja kati ya nchi zinazozalisha kwa wingi katika ukanda huu. Hii itarahisisha bidhaa za Tanzania zinazouzwa chini ya mfumo wa stakabadhi za ghala kuwa na wigo mpana wa ushindani katika ukanda huu.

### *S. Kuimarisha Ushindani wa Kibiashara Nchini*

***146. Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara, kupitia TanTrade, imeendelea kuimarisha uwezo wa wadau wa biashara ili kuongeza ushiriki wao katika shughuli za uzalishaji, uongezaji thamani na upanuzi wa masoko. Katika kipindi hicho, jumla ya wadau wa biashara 1,865 waliwezeshwa kupitia mafunzo ya uanzishaji, usimamizi na uendeshaji wa biashara, masoko pamoja na uongezaji thamani wa bidhaa. Kati yao, washiriki 1,317 walipata mafunzo katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Mbeya, Rukwa, Songwe, Njombe na Mtwara kuhusu usimamizi wa biashara, namna ya kufikia masoko ya ndani na nje ya nchi, matumizi ya fursa za Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA), pamoja na kuongeza thamani ya bidhaa. Aidha, wazalishaji 115 wa viungo walipatiwa mafunzo katika Wilaya ya Muheza, Mkoa wa Tanga. Vilevile, wanafunzi 433 wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) walipatiwa mafunzo kuhusu fursa za biashara zilizopo nchini na katika masoko ya kikanda.

***147. Mheshimiwa Spika;*** TanTrade, imeendelea kuimarisha utambulisho wa bidhaa za Tanzania katika Rajamu ya Taifa (Made in Tanzania) ambapo rajamu hiyo imetekelezwa rasmi na kuanza kutumika katika masoko ya

ndani na nje. Hadi kufikia Aprili, 2026, kampuni 20 zilisajiliwa kutumia rajamu hiyo na bidhaa 58 zilikidhi vigezo vya matumizi yake. Rajamu hiyo ilinadiwa katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, 2025 na katika Mkutano wa 27 wa SADC na kuongeza muonekano wa bidhaa za Tanzania kimataifa.

***148. Mheshimiwa Spika;*** Mamlaka imeendelea kuboresha upatikanaji wa taarifa za biashara ambapo taarifa za bei zilikusanywa kutoka masoko nane (8) ya mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam. Taarifa hizo zilisambazwa kwa jumla ya wadau 75,103 kupitia TanTrade Biashara App, tovuti na mitandao ya kijamii. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya watumiaji 1,460 walikuwa wamejisajili rasmi katika TanTrade Biashara App na kufanikiwa kufuatilia mwenendo wa bei katika masoko 67 nchini. Aidha, tathmini ya fursa za bidhaa za nafaka, nyama na matunda ilifanyika katika masoko ya AfCFTA na EAC ambapo fursa zilionekana zaidi katika nchi za DRC, Uganda, Rwanda, Comoro na Kenya. Taarifa hizo zilisambazwa kwa wafanyabiashara ili kuongeza ushindani wa bidhaa za Tanzania katika masoko ya kikanda.

## *T. Kutafuta Masoko ya Bidhaa za Tanzania Nje ya Nchi*

***149. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea na jitihada za kutafuta na kupanua masoko kwa bidhaa na huduma za Tanzania zinazozalishwa nchini katika masoko ya kimataifa; kutangaza fursa za biashara, uwekezaji na miradi ya kimkakati ya nchi, na kusimamia matukio ya ukuzaji biashara katika kutangaza bidhaa na huduma yaliyoratibiwa na sekta binafsi na Umma kwa lengo la kuimarisha mwenendo wa tasnia ya ukuzaji biashara nchini. Kupitia jitihada hizo, Wizara imefanikiwa kuratibu matukio ya ukuzaji biashara na kuwezesha ushiriki wa wafanyabiashara nchini ili kupata

masoko ya bidhaa na huduma zitolewazo kupitia uratibu na ushiriki wa maonesho; majukwaa ya biashara; mikutano na makongamano; na kupitia mpango wa kuanzisha kitengo cha Intelijensia ya Masoko na Viwanda kama ifuatavyo:

**i. *Maonesho***

***150. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TanTrade) iliratibu Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, mwaka 2025 (49th DITF) yaliyofanyika mwezi Juni hadi Julai, 2025 Dar es salaam. Lengo la maonesho hayo ni kutoa fursa ya kuchochea ukuaji wa biashara na uchumi wa nchi kwa kuwawezesha wazalishaji wa bidhaa na huduma kutangaza na kutafuta masoko endelevu ndani na nje ya nchi. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na maonesho hayo ni ununuzi wa papo kwa papo wenye thamani ya shilingi bilioni 7.06 kutokana na jumla ya watembeleaji 385,500 wa maonesho hayo. Mauzo hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 94.7 ikilinganishwa na mauzo ya papo kwa papo ya shilingi bilioni 3.63 yaliyofanyika katika Maonesho ya 48 Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, mwaka 2024.

***151. Mheshimiwa Spika;*** mafanikio mengine ni kupatikana kwa miadi ya kibiashara yenye thamani ya shilingi bilioni 4.8 iliyofanyika katika sekta za teknolojia, mifugo, usafirishaji, madini, kilimo, uvuvi na ujenzi; uzinduzi wa Rajamu ya Taifa “Made in Tanzania”, na kampuni nane (8) zilisajiliwa kutumia rajamu hiyo. Kampuni hizo ni *Airplanes Africa Limited*, Yusuph Maiko Lehemu (TingaTinga), African Uji Mix, Amir Hamza (T) Ltd, *Tanfoam ltd, Bakhresa Food Products Ltd*, *Soosung Engineering Co.ltd* na Jitegemee Holding Co. Ltd; kupatikana kwa ajira za muda mfupi 22,593 katika kutoa usaidizi wa huduma mbalimbali wakati wa

maandalizi ikiwemo ufundi na ujenzi wa miundombinu na mabanda ya biashara, usafirishaji, migahawa, mapambo na upagaji.

***152. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Tan trade ilisimamia na kuratibu maonesho ya *Tanzania Poultry Show* yaliyofanyika katika Jiji la Dar es Salaam mwezi Oktoba, 2025 ambapo jumla ya kampuni 54 za ndani na nje ya nchi zilishiriki. Kati ya kampuni hizo, kampuni za ndani zilikuwa 30 na 24 za nje. Kampuni hizo zilitoka katika nchi 11 ambazo ni Tanzania, Uholanzi, Ufaransa, India, Ujerumani, Ubelgiji, Kenya, Canada, Hungary, Malawi, na Afrika Kusini. Kupitia maonesho hayo, wadau wa biashara walipata elimu ya teknolojia ya ufugaji wa kuku na ndege wafugwao, namna bora ya ufugaji, elimu ya bima pamoja na elimu ya mikopo kwa wafanyabiashara wa kati na wadogo. Vilevile, TanTrade iliratibu maoesho ya EACLC *Shopping Festival* yaliyofanyika mwezi Agosti, 2025 katika Jiji la Dar es salaam. Kupitia maonesho hayo, jumla ya wafanyabiashara 200 wakiwemo wajasiriamali wadogo walishiriki na kutangaza bidhaa na huduma zao.

***153. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na iliyokuwa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu iliratibu ushiriki wa wajasiriamali katika Maonesho ya 25 ya Wajasiriamali Wadogo na wa Kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki maarufu kama “Nguvu Kazi au Jua Kali” yaliyofanyika Nairobi nchini Kenya mwezi Novemba, 2025. Kupitia maonesho hayo zaidi ya wajasiriamali wadogo na wa kati 300 walipata fursa ya kutangaza bidhaa zao. Kutokana na ushiriki huo, jumla ya mikataba saba (7) ya kibiashara ilisainiwa katika bidhaa za magari, vikapu, nguo, korosho, viungo na nafaka; na mauzo yenye thamani ya shilingi 271,000,000 yalipatikana.

**154. Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia SIDO ilihamasisha wajasiriamali 1,366 kushiriki katika maonesho ya Sabasaba, Nanenane, Maonesho ya Madini, Maonesho ya Wiki ya Chakula na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wajasiriamali hao. Kupitia maonesho hayo, wajasiriamali walikutanishwa na watoa huduma kwa lengo la kuongeza wigo wa soko la bidhaa zao ili kupata wateja wapya; kubadilishana uzoefu na wajasiriamali wengine; na kuunganishwa na wakulima pamoja na taasisi mbalimbali.

***ii. Majukwaa ya Kitaifa na Kimataifa***

**155. Mheshimiwa Spika;** Wizara imefanikiwa kuratibu ushiriki wa Watanzania 175 katika Maonesho ya Dunia ya Expo Osaka Japan 2025 yaliyofanyika Osaka - Japan kuanzia mwezi Aprili hadi Oktoba, 2025. Kupitia jukwaa hilo, jumla ya wageni 4,514,000 walitembelea banda la Tanzania kuanzia mwezi Aprili hadi Oktoba, 2025 ambapo bidhaa 134 za madini na mazao zilinadiwa na kuuzwa. Bidhaa hizo ni pamoja na madini (Tanzanite, Ruby, Garnet), viungo vya chakula, korosho, bidhaa za mkonge na karanga, karafuu, asali, mwani, kahawa na chai. Aidha, miradi ya uwekezaji katika maeneo ya nishati, reli/usafirishaji, kilimo, afya na uchumi wa buluu ilitangazwa. Vilevile, mauzo ya papo kwa papo ya shilingi milioni 300 yalifanyika; na kusainiwa kwa hati za makubaliano nane (8) kati ya Mashirika ya Tanzania na Japan zenye thamani ya shilingi bilioni 38.

**156. Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TanTrade iliratibu ushiriki wa kampuni saba (7) za Kitanzania katika maonesho ya *China International Import Expo (CIIE),* yaliyofanyika Novemba, 2025 Shanghai China. Kampuni hizo ni *Chrises Real Solutions Company Limited, Tingatinga Art Cooperative Society, Swahili Honey, Riyami Resources,*

*Investment Business and Seaweed Development, Tanzanite Love Company Limited* pamoja na *EACLC*. Katika maonesho hayo, bidhaa za madini, mwani, kahawa, asali, parachichi, kokoa, mvinyo, vipodozi na sanaa za mikono zilioneshwa pamoja na kupokea mahitaji ya bidhaa tani 2,000 ikiwemo soya zenye thamani ya shilingi bilioni 1.6.

### *iii. Mikutano na Makongamano*

***157. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imefanikiwa kushiriki katika Kongamano la Biashara kati ya Tanzania na Korea lililofanyika mwezi Novemba 2025. Katika kongamano hilo, jumla ya washiriki 74 walishiriki ambapo kati yao washiriki 59 ni kutoka Tanzania na washiriki 15 ni kutoka Korea. Kongamano hilo liliandaliwa kwa lengo la kuunganisha waagizaji kutoka Korea na wazalishaji wa Tanzania. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na kongamano hilo ni pamoja na kusainiwa kwa hati ya makubaliano kati ya KOIMA na TPSF kwa lengo la kuendeleza mashirikiano ya biashara na uwekezaji; na kupatikana kwa kampuni sita (6) za Tanzania ambazo zinaendelea na mazungumzo ya kibiashara na kampuni kutoka KOIMA-Korea. Makubaliano hayo ni kati ya kampuni za METEL na MEDIPROTECH; KOLMAR BNH,G&S Clearing and Forwading Ltd na CMT Global Logistics; Natureripe Kilimanjaro Ltd na MEDIPROTECH; KOLMAR BNH,TANZANEX Co.Ltd na C.S for life; National Ranching Co.Ltd (NARCO) na Highland Innovation Co.Ltd; pamoja na Union Meat.

### *iv. Kuanzisha Kitengo cha Intelijensia ya Masoko na Viwanda*

***158. Mheshimiwa Spika;*** katika mazingira ya sasa ya ushindani wa kibiashara na viwanda duniani, upatikanaji wa taarifa sahihi, za uhakika na za wakati kuhusu masoko na

teknolojia za viwanda ni suala la muhimu katika maendeleo ya Sekta ya Viwanda na Biashara. Wizara inatekeleza mikakati mbalimbali ya kukuza viwanda na kuongeza mauzo nje ya nchi. Hata hivyo, kumekuwapo na ukosefu wa taarifa za masoko ya kimataifa; kutokujua bidhaa zinazohitajika katika misimu ya mahitaji, viwango vya ubora na vikwazo vya kibiashara (tariffs & NTBs); na ugumu wa kutofautisha wawekezaji makini na wale wenye nia ya "dumping", pamoja na ukosefu wa taarifa za uwezo wao wa kifedha na teknolojia. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imedhamiria kuanzisha Kitengo cha Intelijensia ya Masoko na Viwanda.

***159. Mheshimiwa Spika;*** kitengo hicho kitatekeleza majukumu ya kukusanya na kuchambua taarifa za masoko ya kimataifa; kubaini fursa za bidhaa, mwenendo wa mahitaji na vigezo vya kuingia sokoni; kuandaa na kusambaza taarifa za fursa za masoko kwa wafanyabiashara; na kutoa taarifa za tahadhari za haraka kuhusu mabadiliko ya masoko. Kuanzishwa kwa kitengo hicho ni hatua muhimu katika kujenga uchumi wa viwanda unaotegemea taarifa sahihi.

### ***U. Kusimamia na Kuimarisha Mifumo ya Ufanyaji Biashara***

***160. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TanTrade imehuisha taratibu za uondoshaji wa bidhaa saba (7) kupitia Bandari ya Dar es Salaam, ambazo ni parachichi, mihogo, ngozi, kokoa, viungo, nafaka na uyoga. Bidhaa hizo zimewekwa katika Mfumo wa Trade Portal (trade.tanzania.go.tz) ili kuongeza uwazi, kupunguza muda wa kufuata taratibu na kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wafanyabiashara wa ndani na nje. Aidha, taarifa za taasisi wezeshi mbili (2) za Zanzibar ambazo ni *Zanzibar State Trade Corporation* na *Zanzibar Seaweed Company*; na Wizara ya

Biashara na Maendeleo ya Viwanda zilihuishwa katika mfumo huo ili kuboresha usomaji wa mifumo na kuimarisha utoaji wa huduma za biashara ya kimataifa.

### *V. Kuchunguza Mashauri ya Ushindani*

***161. Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) imeshughulikia mashauri 43 ya ushindani sokoni. Kati ya mashauri hayo, mashauri 38 yanahusu miungano ya kampuni ambayo haikutolewa taarifa FCC na mashauri matano (5) yanahusu matumizi mabaya ya nguvu ya soko. Kati ya mashauri 38 yanayohusu miungano ya kampuni ambayo hayakutolewa taarifa FCC, uamuzi wa mwisho umetolewa kwenye mashauri manne (4), mashauri 18 yameshatolewa uamuzi wa awali na uchunguzi kwenye mashauri 16 bado unaendelea. Kwa upande wa matumizi mabaya ya nguvu ya soko, uchunguzi kwenye mashauri manne (4) yanayohusiana na uzalishaji na usambazaji wa madaftari, sarufi, sigara na bia yanaendelea na uamuzi wa awali umetolewa kwenye soko la usambazaji wa vinywaji baridi nchini.

***162. Mheshimiwa Spika;*** kati ya mashauri matano (5) yanayohusu makubaliano yanayokatazwa na Sheria ya Ushindani, (FCC) inaendelea na hatua ya utekelezaji (Enforcement) katika mashauri mawili (2) yanayohusu soko la uzalishaji na usambazaji wa nondo na soko la uingizwaji na usambazwaji wa magari mapya nchini na inatarajia kutoa maamuzi ya mwisho kwa Wadau wa mashauri hayo. Pia FCC imekamilisha uchunguzi kwenye soko moja (1) la uzalishaji na usambazaji wa saruji nchini na inatarajia kutoa maamuzi ya awali kwa Waadawa husika. Mashauri mawili (2) yanayohusu masoko ya mbolea na kakao yapo katika hatua ya uchunguzi na ukusanyaji wa taarifa unaendelea.

### *W. Kuchunguza Maombi ya Miungano ya Kampuni*

***163. Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) imeshughulikia jumla ya maombi ya Miungano ya Kampuni 62, maombi hayo yalitoka katika sekta za uzalishaji (13); utalii (3); madini (5); bima (8); usafirishaji (6); nishati (4); Michezo (4): benki (2); Afya (4); kilimo (6); ardhi na nyumba (2); mawasiliano (4); Ujenzi (1). Kati ya maombi hayo, maombi 37 yaliidhinishwa bila masharti baada ya Tume kujiridhisha kuwa miungano hiyo haitakuwa na athari hasi za kiushindani. Maombi manne (4) yaliidhinishwa kwa masharti mahsusi ili kuhakikisha kampuni zinazoungana haziathiri ushindani sokoni.

***164. Mheshimiwa Spika;*** kwa upande wa maombi 21 yaliyobaki yapo katika hatua mbalimbali za uchunguzi na yanatarajiwa kutolewa maamuzi katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025/2026. Miungano hii imeendelea kuleta faida katika ukuaji wa sekta mbalimbali kwa kukuza mitaji na teknolojia, kuwezesha upatikanaji wa masoko na kuongeza ajira kwa watanzania. Mathalan, kununuliwa kwa hisa asilimia 65 za Hospitali ya Regency na kampuni ya Tasakhtaa Hospital Limited imesaidia kukua kwa mtaji na upanuzi wa soko katika Sekta ya Afya. Vilevile, FCC kwa kushirikiana na BRELA, ilifanya upekuzi wa jumla ya kampuni 1,214 katika Kitabu cha Msajili wa Makampuni. Lengo la upekuzi huo ni kujiridhisha kuwa kampuni hizo zilizofanya mabadiliko ya muundo wa udhibiti wa kampuni, yalitekelezwa bila kuathiri utekelezaji wa vifungu vya Sheria ya Ushindani.

### *X. Kuendelea Kuchukua Hatua dhidi ya Bidhaa Bandia na Kumlinda Mlaji*

***165. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia FCC imeendelea na juhudi za kupambana na bidhaa bandia na kumlinda mlaji dhidi ya mienendo potofu, hadaifu na kandamizi katika soko la bidhaa na huduma. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia FCC imeshughulikia malalamiko 63 ya walaji wadogo ambapo malalamiko 45 yalipatiwa ufumbuzi na malalamiko 18 yaliyobaki yapo katika hatua mbalimbali za utatuzi; imesajili na kuthibitisha mikataba 27 inayoandaliwa na upande mmoja (SFCC) kwa lengo la kuondoa masharti kandamizi kwa walaji; imefanya kaguzi za kushtukiza 31 ambapo bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 4.74 zilikamatwa kwa kuvunja Sheria ya Alama za Bidhaa ya 1963 (kama ilivyorekebishwa). Bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na vipuri vya magari, vilainishi vya magari, pombe kali, vyandarua, dawa za viatu na betri. Vilevile, imeendelea na ukaguzi wa kila siku wa mizigo (cargoes) ya bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia Bandari na Bandari kavu zote (ICDs) na vituo vya pamoja vya mipakani. Kati ya mizigo ya bidhaa 4,791 iliyokaguliwa, mizigo ya bidhaa 418 ilikamatwa kwa kukiuka Sheria ya Alama za Bidhaa Sura ya 85.

***166. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia FCC imeendelea kutekeleza mkakati unaohusisha matumizi ya teknolojia za ukaguzi wa bidhaa, utoaji wa elimu kwa umma na kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za serikali, sekta binafsi na wananchi ili kuhakikisha udhibiti endelevu wa bidhaa bandia, kulinda afya ya wananchi, kuongeza mapato ya Serikali na kuimarisha ushindani wa haki katika soko.

### *Y. Kutoa Maamuzi ya Mashauri ya Rufaa Yanayowasilishwa Katika Baraza la Ushindani*

***167. Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia Baraza la Ushindani (FCT) imepokea na kutoa maamuzi ya mashauri 25 yaliyokuwa tayari kwa ajili ya usikilizwaji. Mashauri hayo yanajumuisha rufaa zinazotokana na maamuzi ya mamlaka mbalimbali za udhibiti na ushindani nchini, ikiwemo mashauri yanayohusu ukiukwaji wa sheria za ushindani, matumizi mabaya ya nguvu ya soko, miunganiko ya kampuni (mergers and acquisitions), bidhaa bandia, migogoro ya leseni na tozo za huduma zinazodhibitiwa na mamlaka za kisekta. Matokeo ya maamuzi ya mashauri hayo yameongeza na kuchangia uwajibikaji katika soko; uwajibikaji kwenye ushindani katika sekta ya viwanda na biashara; kampuni kuongeza umakini katika kufuata sheria za nchi; kuongezeka kwa uwazi na ushindani wa bei katika kampuni mbalimbali nchini; ufanisi katika uzalishaji; usambazaji wa huduma na bidhaa; kukuza ubunifu; na kumlinda mlaji.

### *Z. Usimamizi na Uhakiki wa Vipimo Vitumikavyo na Viingiavyo Nchini*

***168. Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo (WMA) imekagua na kuhakiki vipimo 995,884 sawa na asilimia 112.5 ya lengo la kukagua vipimo 885,307. Kati ya vipimo vilivyokaguliwa na kuhakikiwa, vipimo 30,512 vilirekebishwa na vipimo 713 vilikataliwa. Aidha, Wakala iliendelea kufanya kaguzi za kawaida na za kushtukiza ambapo jumla ya kaguzi 4,192 sawa na Asilimia 104.8 zilifanyika kati ya kaguzi 4,000 zilizopangwa kufanyika.

**169. Mheshimiwa Spika;** vipimo vilivyokaguliwa kwa wingi ni Pampu za kuuzia mafuta ya nishati; *Flowmeters* zitumikazo kupimia mafuta kwenye bohari na maghala ya kuhifadhia mafuta; tenki za kusafirishia mafuta na tenki za kuhifadhia mafuta; mita za maji; mizani inayotumika kupimia bidhaa mbalimbali; vipimo vya urefu; na malori yabebayo kokoto, mchanga na vifusi. Vilevile, uhakiki na ukaguzi ulifanyika kwenye maeneo mbalimbali yakiwemo masoko ya nafaka, vituo vya mafuta, bohari/maghala ya mafuta, sehemu za kuuzia mbao, bucha na maduka ya kuuzia bidhaa mbalimbali.

**170. Mheshimiwa Spika;** kaguzi na ufuatiliaji wa uhakiki wa vipimo vinavyotumika katika ushushaji wa mafuta jamii ya petroli pamoja na mafuta ya kula ulifanyika. Kupitia kaguzi hizo, jumla ya meli 116 zilizoingia nchini zenye jumla ya lita bilioni 7.97 zilikaguliwa ambapo kati ya lita hizo, lita bilioni 2.43 zilikuwa petroli, lita bilioni 4.95 dizeli, lita bilioni 0.35 mafuta ya taa na lita bilioni 0.25 mafuta ya kula. Aidha, taarifa inayotokana na ukaguzi hutumiwa na Mamlaka nyingine za Serikali kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya utozaji wa kodi, EWURA kwa ajili ya upangaji wa bei za mafuta, Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa ajili ya wanunuzi na wauzaji wa mafuta pamoja na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

### AA. Ukaguzi wa Bidhaa Zilizofungashwa Kwenye Maeneo ya Mipakani, Bandarini na Viwandani

**171. Mheshimiwa Spika;** Wakala imeendelea kufanya kaguzi za bidhaa zilizofungashwa kwenye maeneo ya mipaka ya kivipimo ya Sirari Mkoa wa Mara; Mtukula, Kagera; Namanga, Arusha; Holili na Tarakea, Kilimanjaro; Tunduma, Songwe; Horohoro, Tanga; Kasumulu, Mbeya; Manyovu,

Kigoma; Kwala, Pwani; Mbweni, Dar es Salaam; na maeneo ya viwandani. Ukaguzi huo ulilenga kuhakiki usahihi wa kiasi/ idadi iliyotamkwa (declared quantity). Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya shehena 13,458 zenye bidhaa 16,768 zilikaguliwa na kuhakikiwa, ikilinganishwa na lengo la shehena 16,180 zenye bidhaa 17,774 zilizokadiriwa kuingia nchini. Vilevile, kulifanyika uhakiki wa bidhaa zinazozalishwa na kufungashwa na viwanda vya ndani, ambapo jumla ya bidhaa 18,296 zilikaguliwa ikilinganishwa na lengo la kukagua bidhaa 17,990.

***172. Mheshimiwa Spika;*** bidhaa ambazo hazikidhi matakwa/vipimo adhabu hutolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 46 cha Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 ambapo, hupigwa faini na kuamriwa bidhaa hizo kuteketezwa kwa kukatwakatwa mbele ya wakaguzi, kisha kurudishwa kwa mzalishaji ili zitengenezwe upya kwa vipimo sahihi. Aidha, watuhumiwa wanaofikishwa mahakamani hupewa adhabu kwa mujibu wa Kifungu cha 45 cha Sheria hiyo au kutaifishwa kwa bidhaa hizo kwa mujibu wa Kifungu cha 50.

### *BB. Kuboresha Mazingira ya Utendaji Kazi pamoja na Ununuzi wa Vifaa vya Kisasa vya Uhakiki wa Vipimo*

***173. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi ya WMA kwa kuanza mchakato wa ujenzi wa Ofisi za Wakala katika mikoa ya Lindi na Songwe. Hadi kufikia Aprili, 2026, usanifu na michoro ya majengo umekamilika. Hatua inayofuata ni kutangaza zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi. Sambamba na hilo, Wakala imenunua vifaa vya kisasa vya uhakiki wa vipimo ikiwa ni pamoja na vifaa vya TEHAMA (Laptop 35, Desktop 28, Scanner 2, Multifuctional printer 20, Photocopier 2, Colour printer 1). Vilevile, Wakala imekamilisha ununuzi wa vifaa vya

kitaalam ambavyo ni:- *Digital Thermometer 1, CNG Dispensing Pump Verifier 2, Electronic Balances 31, Mass comperator 2, Flow Meters 4, Proving Tanks 11, Preasure Gauges 9, Portable Legal Metrology Test Kit for Field Inspectors 40,* na *Legal Metrology Test Kits for Verifying High-Precision Balances 20.* Upatikanaji wa vifaa hivyo utaongeza wigo wa uhakiki wa vipimo katika maeneo mapya na kuweza kutoa huduma kwa karibu zaidi.

### CC. *Kukabiliana na Changamoto ya Lumbesa*

***174. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia WMA, ina jukumu la kusimamia na kuhakikisha matumizi sahihi ya vipimo katika biashara na uchumi ili kulinda Wakulima, Wauzaji, Wanunuzi na Wasafirishaji wa mazao shamba. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeendelea kufuatilia mwenendo wa biashara ya mazao ya kilimo nchini, na imebaini kuendelea kuwepo kwa vitendo vya ufungashaji na uuzaji wa mazao hayo kinyume na taratibu za Sheria ya Vipimo Sura ya 340, maarufu kama *"Lumbesa."* Sheria, hiyo pamoja na mambo mengine inaeleza kuwa mazao yaliyofungashwa kwa namba/idadi/uzito hayapaswi kuzidi kilogramu 100 pamoja na kiasi himilivu cha asilimia 5 (Tolerance limit of +5 %) na imeelekeza wauzaji/wanunuzi wa mazao kutumia mizani ambayo kwa mujibu wa Sheria inapaswa kuhakikiwa na Wakala wa Vipimo angalau mara moja kwa mwaka.

***175. Mheshimiwa Spika*;** katika jitihada za kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imefanya jitihada mbalimbali kwa kufanya operesheni tisa (9) katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Pwani, Morogoro, Mbeya, Iringa, na Njombe. Kupitia operesheni hiyo, magari 2,500 yanayosafirisha mazao yalikaguliwa, kati ya hayo magari

2,419 yalikuwa na mazao yaliyofungashwa kwa uzito unaoruhusiwa yaani usiozidi kilogramu 100 na magari 81 yalikutwa na makosa kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Sura ya 340 na hatua stahiki zilichukuliwa kwa wahusika ikiwa ni pamoja na kutozwa faini ya papo kwa papo na kuamriwa kufungasha upya.

***176. Mheshimiwa Spika*****;** operesheni hizo ni endelevu na zinafanyika mikoa yote Tanzania Bara kupitia Ofisi za Mikoa za Wakala wa Vipimo zilizopo nchi nzima ili kutokomeza kabisa changamoto hiyo. Vilvevile, Serikali imesogeza huduma ya uhakiki wa vipimo kwa wananchi kwa kuweka vituo vya muda 5,050 katika maeneo ya ofisi za Kata, Mitaa na Vijiji. Aidha, baadhi ya Halmashauri za miji na Wilaya kama vile Mpanda, Kasulu na Kibondo zimetunga sheria ndogo za ushuru wa mazao zikisisitiza upimaji wa mazao kufanyika kwa kutumia mizani iliyohakikiwa na Wakala wa Vipimo.

### *DD. Kuboresha Miundombinu ya Kufundishia na Kujifunzia katika Chuo cha CBE*

***177. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) inaendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa 10 la *Metrology Complex* katika Kampasi ya Dar es Salaam. Hadi kufikia Aprili, 2026 ujenzi umefikia asilimia 93, ambapo shilingi bilioni 8.88 zimetumika kati ya shilingi bilioni 10.39 zilizotengwa kwa hatua ya kwanza. Jengo litakapokamilika litakuwa na kumbi 29 za mihadhara zenye uwezo wa kubeba wanafunzi 4,160, hivyo kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

***178. Mheshimiwa Spika;*** ujenzi wa miundombinu umeenda sambamba na maboresho ya mitaala na programu

ili kuongeza kiwango cha udahili. Wizara kupitia CBE imeboresha mitaala ili kukidhi mahitaji ya soko na maendeleo ya teknolojia, ikisisitiza elimu ya vitendo kupitia Programu ya Uanagenzi, ambapo wanafunzi watatumia nusu ya muda darasani na nusu kazini kupata uzoefu halisi wa kazi. Hadi kufikia Aprili, 2026 mitaala mipya nane (8) imeidhinishwa na kufanya jumla ya mitaala iliyopitishwa kufikia 71. Aidha, mitaala mingine 28 ipo katika hatua za maandalizi na uthibitishaji. Ongezeko la mitaala hiyo limepelekea kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi na hivyo kuhitaji miundombinu toshelevu ya kufundishia na kujifunzia. Mathalan, mwaka wa masomo 2023/2024 udahili ulikuwa wanafunzi 20,029 ikilinganishwa na wanafunzi 24,957 katika mwaka wa masomo 2025/2026 sawa na ongezeko la wanafunzi 4,928.

**EE. *Uendelezaji wa Bunifu Kupitia Programu Atamizi***

***179. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TEMDO imeendelea kuwasaidia wajasiriamali wabunifu kwa kuwawezesha kupata huduma kama vile maeneo ya kufanyia kazi; mashine na mitambo; ushauri wa kiufundi; na kuwaunganisha na taasisi za kifedha ili wakue na kufikia viwango vya kujitegemea. Hadi kufikia Aprili, 2026 wajasiriamali wabunifu watano (5) ambao ni *Bivac Co. Ltd, Rest Food Process Ltd, Upendo Food Process Ltd, Simba and Alice Food Process Ltd* na *Neema Nafaka Products* wameendelea kuzalisha bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo kwenye kiatamizi cha TEMDO katika Mkoa wa Arusha ambapo ajira 220 zimezalishwa. Kati ya ajira hizo, ajira za moja kwa moja ni 100 na ajira zisizo za moja kwa moja ni 120. Baadhi ya bidhaa zinazozalishwa ni pamoja na siagi ya karanga, unga lishe, vyakula lishe, biskuti na virutubisho mbalimbali.

***180. Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara kupitia SIDO imekamilisha jumla ya mawazo bunifu nane (8) kati ya 24 na yapo kwenye majaribio ya kufanya biashara (commercialization) chini ya uangalizi wa SIDO. Mawazo bunifu hayo ni utengenezaji wa kifaa cha kuuza maji kwa kuweka sarafu; utengenezaji wa taulo za kike zenye uwezo wa kutumika tena; utengenezaji wa vichocheo (booster) za mbolea kwa kutumia mabaki ya nywele za binadamu; akili unde inayoendesha vifaa vya kielektroniki vya nyumbani; utengenezaji wa sabuni za asili na mimea; utengenezaji wa vifaa vya maabara ya shule kwa ajili ya mafunzo ya sayansi kwa vitendo; utengenezaji wa mikate na bidhaa nyingine zilizorutubishwa; na utengenezaji wa mabegi ya shule yenye *solar charge*. Aidha, mawazo bunifu 16 yaliyosalia yanaendelea kuatamiwa katika mkoa wa Dar es salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Iringa, Singida na Morogoro.

***181. Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia TIRDO ina jumla ya wabunifu 23 wanaoatamiwa ambapo kupitia wabunifu hao, kampuni 10 tayari zimeanzishwa na kusajiliwa rasmi. Kampuni hizo ni *Plant Biodefender Ltd (Moshi), PREYO Company Ltd, Innovex Solutions and Merchants, H.O.P Electronics Technologies, Innovasie Company Ltd, Albetus Technologies, Ammacom Technologies Co. Ltd, Survey Fish Market Company, Munny Chocolate Company Ltd,* na *Kaypee Motors Ltd.* Wabunifu hao wamewezeshwa kwa kupewa maeneo ya uzalishaji kupitia mpango wa uatamiaji. Aidha, Shirika linaendelea kuwasaidia katika kuboresha ubora wa bidhaa, kuthibitisha viwango na kuwaunganisha na taasisi za kifedha ili waweze kupata mitaji ya kuendeleza shughuli zao.

***182. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia CBE imeendelea kutoa mafunzo ya atamizi za biashara kwa lengo la kutoa mazingira bora ya kukuza bunifu za kibiashara; na kuwajengea vijana uwezo wa kiutendaji na kuwaunganisha na fursa za soko, mitaji na ushauri wa kitaalamu ili kusaidia ukuaji na maendeleo ya biashara hususan biashara changa (Start-ups). Mafunzo hayo yamegawanyika katika hatua tatu (3) ambazo ni hatua kabla ya atamizi (pre- incubation); atamizi (incubation) na baada ya atamizi (post- incubation). Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya bunifu 773 zimesajiliwa katika atamizi za biashara na teknolojia za chuo. Kati ya hizo, 278 sawa na asilimia 36 zipo katika hatua ya maandalizi; 75 sawa na asilimia 9.7 zipo kwenye atamizi; na 420 sawa na asilimia 54.3 zipo katika hatua ya baada ya atamizi.

### *FF. Elimu na Mafunzo*

***183. Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha mwaka 2025/2026, Wizara imetoa elimu na mafunzo kwa umma na wajasiriamali. Elimu iliyotolewa ilihusu viwango na udhibiti ubora; urasimishaji wa biashara; matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala; matumizi sahihi ya vipimo; na teknolojia. Elimu na mafunzo yaliyotolewa katika maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

#### i. *Teknolojia ya Kuongeza Virutubisho Kwenye Vyakula*

***184. Mheshimiwa Spika;***. hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara imetoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati 78 wanaojihusisha na usindikaji wa vyakula hususan unga wa mahindi, mafuta, chumvi na ngano katika mikoa ya Simiyu na Shinyanga. Lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha wajasiriamali hao wanatumia teknolojia ya uongezaji wa

virutubishi katika vyakula hivyo ili viweze kukidhi soko la ndani na nje. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa wajasiriamali kuhusu ujasiriamali, uendeshaji biashara na ujuzi maalum wa kiufundi katika uzalishaji.

**_185._** ***Mheshimiwa Spika;*** mafunzo mengine yalilenga masuala ya KAIZEN, utengenezaji sabuni, batiki, vipodozi, usalama viwandani, ufungashaji na usimamizi wa mikopo ambapo Wanawake 5,604 sawa na asilimia 68 na Wanaume 2,638 sawa na asilimia 32 walishiriki. Kutokana na mafunzo hayo jumla ya biashara ndogo na za kati 646 zilirasimishwa katika maeneo ya usindikaji vyakula, utengenezaji sabuni na utengenezaji batiki. Halikadhalika ushauri kuhusu umuhimu wa kurasimisha biashara ulitolewa kwa wajasiriamali kwa ushirikiano na Mamlaka za Serikali za Mitaa, BRELA, TBS, GCLA na TRA.

### *ii. Mafunzo na Semina Kuhusu Viwango na Udhibiti Ubora*

**_186._** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TBS imeendelea kutoa elimu kwa wazalishaji wa bidhaa za viwandani, wasindikaji na umma wa watanzania kuhusu dhana nzima ya viwango na ubora. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya wadau 1,215 wa sekta tano (5) ndogo za vifungashio, matofali, vipodozi, unga wa mahindi na vyakula vya mifugo walipewa mafunzo juu ya masuala ya viwango ambayo ni sawa na asilimia 67.5 ya lengo la kutoa mafunzo kwa wadau 1,800 kwa mwaka mzima. Mafunzo hayo yalifanyika katika Mikoa ya Dodoma, Iringa, Singida, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Pwani, Morogoro, Dar es Salaam, Geita, Shinyanga, Simiyu, Mara, Mwanza, Rukwa, Songwe, Mbeya na Ruvuma. Aidha, Shirika limeendelea kutoa mafunzo hayo kwa wajasiriamali wadogo (SMEs) na wadau mbalimbali

katika dhana nzima ya kuwawezesha kuzalisha bidhaa zinazokidhi matakwa ya viwango vya ubora na usalama ili kuwezesha kukidhi ushindani wa masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.

### *iii. Ugani na Mafunzo ya Zana za Kilimo na Teknolojia za Vijijini*

***187. Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea na shughuli za ugani na mafunzo yenye lengo la kukuza matumizi ya teknolojia mbalimbali kwa maendeleo ya viwanda. Wizara kupitia CAMARTEC imetoa mafunzo ya matumizi ya teknolojia za viwandani kupitia Vitovu vya Teknolojia za Kihandisi (VITEKI) vya Maswa na Karatu, ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 vijana 78 wamepata elimu ya kutumia mashine za kupura mazao (mtama, mahindi, mbaazi na alizeti) na kukamua mafuta ya alizeti. Pia, kupitia Kiwanda Darasa cha Kubangua Korosho Manyoni, vijana 16 hususan wanawake wamefundishwa kubangua na kufungasha korosho kwa ajili ya soko la ndani na nje. Vilevile, mafunzo ya kuchakata siagi ya karanga yametolewa kwa wajasiriamali wanne (4) katika Kiwanda Darasa cha Nzega.

### *iv. Uhamasishaji Matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala*

***188. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia WRRB imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Hadi kufikia Aprili, 2026 Bodi imefanikiwa kutoa elimu kwa wadau wa mfumo 1,488,584 kupitia mikutano ya wadau, ushiriki wa maonesho na makongamano ya kitaifa na kimataifa, kurasa za mitandao ya kijamii na vyombo vya Habari. Kati ya wadau hao, wadau 1,487,608 walipata elimu kupitia mitandao ya kijamii, wadau

289 kupitia maonesho ya Sabasaba, wadau 200 kupitia maonesho ya Nane Nane, na wadau 487 kupitia mikutano ya wadau mbalimbali.

### *v. Elimu kuhusu Haki katika Ushindani wa Soko*

***189. Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia FCT imefanya semina katika mikoa 10 ya Mbeya, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Shinyanga, Kigoma, Mtwara, Lindi, Dodoma na Dar es Salaam na kuwajengea uwezo wadau 3,000 kutoka sekta ya biashara/wawekezaji, wakulima, watoa huduma, walaji na watumishi wa umma. Mafunzo hayo yalilenga kuongeza uelewa katika masuala yanayohusu ushindani wa kibiashara; udhibiti wa soko; na matumizi ya mfumo wa kusajili mashauri kwa njia ya kieletroniki.

### *vi. Elimu kwa Umma Kuhusu Matumizi Sahihi ya Vipimo*

***190. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia WMA imeendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya vipimo kwa wadau mbalimbali wakiwemo wakulima, Umoja wa wamiliki wa Viwanda vya Alizeti Kongwa, wafanyabiashara, wasafirishaji, mafundi miundo na wauzaji wa mafuta. Elimu hiyo imetolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo programu 100 za luninga (TV), stori za Blogu 230, maonesho matano (5) ambayo ni Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (Saba Saba), Nanenane, Maonesho ya Madini Geita, Maonesho ya TCIAA Mwanza, na Maonesho ya Usafirishaji Dar es Salaam. Aidha, jumla ya wadau 3,970 walitembelea mitandao ya kijamii na kupata mafunzo hayo.

### vii. *Elimu Kuhusu Usindikaji wa Nafaka, Vipodozi na Uzalishaji wa Bidhaa Bora za Ngozi*

***191. Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TIRDO ilitoa mafunzo kwa wadau wa viwanda Wadau hao ni pamoja na wajasiriamali 20 wa utengenezaji wa mkaa (*briquette),* wadau 41 wa uzalishaji bora wa mkaa mbadala na uhakiki wa ubora, wadau 94 wa usindikaji wa nafaka na vipodozi kutoka katika viwanda 94 katika Manispaa za Tabora na Mpanda, Katavi na wadau 23 wa uzalishaji wa bidhaa bora za ngozi kutoka mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Kilimanjaro na Morogoro. Aidha, huduma za kitaalam zilitolewa kwa viwanda mbalimbali ikiwemo Tanzania Pharmaceutical Industries Limited (TPI), MSD Makambako na Kilimanjaro International Leather kwa kusimamia ujenzi wa kiwanda hicho na kuwezesha kufanya majaribio ya awali, hatua iliyochangia kuimarisha ubora wa uzalishaji, kuongeza tija na ushindani wa bidhaa za viwandani nchini.

### *viii. Mafunzo ya Muda Mfupi kwa Wajasiriamali*

***192. Mheshimiwa Spika;*** hadi kufikia Aprili,2026, Wizara kupitia CBE imetoa mafunzo ya kozi 20 za muda mfupi kwa wajasiriamali 1,240 katika mikoa ya Mwanza (440) na Mbeya (800). Mafunzo hayo yalihusu Utunzaji wa Taarifa za Kifedha (Financial Records Keeping) na Elimu ya Mlipa kodi (Tax payment edeucation). Lengo la mafunzo ni kuwajengea uwezo wajasiriamali ili waweze kusimamia na kukuza shughuli zao kwa ufanisi zaidi, ikiwemo usimamizi wa biashara na ukuzaji wa mitaji.

## 4. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2026/2027

***193. Mheshimiwa Spika;*** Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2026/2027 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo: Dira 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 - 2030/2031); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025; Sera na Sheria mbalimbali; Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2026/2027 - 2030/2031; Maoni na Ushauri wa Kamati za Kudumu za Bunge na maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

### 4.1 Vipaumbele

***194. Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele kama ifuatavyo:-

i. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati ya Viwanda;

ii. Kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma kwa kuboresha mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kongani (Industrial Clusters) na mitaa ya viwanda (Industrial Estates) kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati;

iii. Kuchochea maendeleo ya viwanda na biashara kupitia ubunifu na matumizi ya teknolojia za kisasa, elimu na mafunzo ya ujuzi.

iv. Kuimarisha upatikanaji wa fedha na mitaji kwa wajasiriamali na wazalishaji viwandani;

v. Kuboresha mazingira ya biashara na kuchochea ukuaji wa Sekta binafsi;

vi. Kuendelea na utafutaji wa masoko kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini; na

vii. Kuanzisha na kuendeleza mawazo ya biashara na bunifu (Innovation and Business Hubs) kwa vijana kwa lengo la kuchochea uchumi.

